

# Liahona

**Kristo  
Aliye Hai**  
NA UREJESHO  
**unaoendelea**

Rais Nelson: Siku za  
Baadaye za Kanisa,  
ukurasa wa 6

Nafasi Yako katika  
Urejesho Unaoendelea,  
ukurasa wa 18

Pasaka katika Kitabu  
cha Mormon,  
kurasa 24, 28

VENITE A ME

MATTEO 11:28


KANISA  
LIKO  
HAPA

# Nairobi Kenya






Wakati Urejesho unaoendelea unapoendelea, injili inapatikana kote ulimwenguni. Kenya ni mfano wa ukuaji wa Kanisa katika Afrika.

waumini  **14,143**

**2**  vingingi

mikusanyiko  **48**

**1**  misheni

vituo vya historia ya familia  **5**

**78**  asilimia ya idadi ya watu ni Wakristo

**1979** Waongofu wa kwanza kutoka eneo husika wanajiunga na Kanisa.

**1988** Mfungo maalum unachangisha fedha za kutuliza kiangazi katika vijiji 15.

**2001** Kigingi cha Nairobi kinaanzishwa.

**2020** Ofisi za eneo Nairobi zinaanza kufanya kazi kikamilifu, zikihudumia waumini 100,000 katika mataifa 18 ya Afrika ya kati.



PICHA KUTOKA GETTY IMAGES



### Siku za Baadaye za Kanisa

*Rais Russell M. Nelson*

6



Kuhudumu kupitia  
Mkutano Mkuu


14



### Urejesho Unaoendelea

*Na Mzee LeGrand R. Curtis Jr.*

18



Pasaka Ina  
Maana Gani  
Kwangu  
Mimi?

28

## Miaka 200 ya Nuru

Siku moja nzuri, angavu miaka 200 iliyopita, mvulana mmoja aliingia katika msitu akiwa na nia ya kutafuta msamaha na kusali kuhusu kanisa ambalo angejiunga nalo. Kutokana na ono la kimiujiza, alijifunza kwamba asijiunge na lolote. Hivyo kuashiria mwanzo wa Urejesho wa injili ya Yesu Kristo—mchakato ambao unaendelea katika siku yetu.

Katika toleo hili, tunasherehekea miaka 200 ya Nuru:

- Rais Russell M. Nelson anafundisha jinsi kukusanya Israeli kutoka pande zote mbili za pazia kunavyoweza kututayarisha sisi pamoja na wengine kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Bwana (ukurasa wa 6).
- Mzee LeGrand R. Curtis Jr. anaonesha jinsi ambavyo Watakatifu wa Siku za Mwisho wamechangia kwenye Urejesho unaoendelea—na jinsi kila mmoja wetu anavyoweza kuchangia (ukurasa wa 18).
- Kwa ajili ya vijana, Mzee Neil L. Andersen anashiriki kweli tano tunazoweza kujifunza kutokana na Ono la Kwanza (ukurasa wa 52).

Tunapojifunza kutoka kwenye maneno ya nabii wetu na hadithi za Watakatifu waaminifu, na tuweze kuja kwenye ufahamu sawa na ule ambao Nabii Joseph alipata kuelewa miaka 200 iliyopita: kwamba Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo ni viumbe wa kweli, wanaoishi ambao wanatupenda. Na tushiriki ufahamu huo pamoja na marafiki na majirani zetu.

Wenu waaminifu,  
Mzee Randy D. Funk wa Sabini  
Mhariri wa Magazeti ya Kanisa

# Yaliyomo

## 5 Mkutano Mkuu miaka yote 🕒

### 6 Siku za Baadaye za Kanisa

*Na Rais Russell M. Nelson*

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho linautayarisha ulimwengu kwa ajili ya kurudi kwa Mwokozi.

### 12 Taswira za Imani 🕒

**Berglind Guðnason**

Wakati mapambano yake na mfadhaiko yalipokuwa magumu kustahimili, Berglind alizungumza kuhusu mapambano yake, na Baba wa Mbinguni alimsaidia kupona.

### 14 Kanuni za Kuhudumu

**Kuhudumu kupitia Mkutano Mkuu**

Mkutano mkuu unatupatia njia nyingi za kuhudumu—kabla, wakati wa, na baada ya wikiendi ya mkutano mkuu.

### 18 Urejesho Unaoendelea

*Na Mzee LeGrand R. Curtis Jr.*

Urejesho ulianza katika Msitu Mtakatifu miaka 200 iliyopita, na unaendelea leo.

### 24 Walikuwa na Tumaini la Kuja kwa Kristo

**—na Pia Sisi Tunaweza Kuwa Nalo 📖 🕒**

*Na Mindy Selu*

Tunaweza kuwa na tumaini katika Ujio wa Pili wa Kristo kwa namna sawa na vile walivyofanya manabii katika Kitabu cha Mormoni.

### 28 Njoo, Unifuute: Kitabu cha Mormoni 📖 🕒

Tumia makala haya ya kila wiki kuboresha kujifunza kwako Kitabu cha Mormoni mwezi huu.

### 32 Sauti za Watakatifu wa Siku za Mwisho 🕒

Baba anampa binti yake zawadi ya thamani kubwa; mama anayeomboleza anakumbushwa kuhusu neema ya Mungu; dada anatafakari juu ya thamani ya nafsi; imani ya mvulana inasaidia familia yake.

### 36 Masomo kutoka Kitabu cha Mormoni 📖 🕒

**Badiliko Kuu la Moyo**

*Na Mzee Kyle S. McKay*

Wakati tunapotubu, Upatanisho wa Mwokozi unaweza kusababisha ndani yetu badiliko kuu la moyo.

### 40 Kuboresha Uzoefu Wetu wa Hekaluni 🕒

*Na Urais wa Kwanza*

🕒 Kupitia kwa Haraka

📖 Msaada wa *Njoo, Unifuute*



**Juu ya Jalada**  
Picha na  
Stefano Cirianni

# Sehemu

## Vijana Wakubwa

# 42

Vijana Wakubwa ni **sehemu muhimu ya Urejesho Unaoendelea.**

Jifunze jinsi ambavyo unaweza kutoa msaada!




## Vijana

# 50

Ono la Kwanza ni **ushahidi wa upendo wa Mungu** kwa wato-

to Wake—hasa kwa wale wana-omtafuta Yeye.



## Watoto

# Rafiki

Kanisa la Yesu Kristo limerejeshwa!



## MAKALA YA KIDIJITALI-PEKEE YA APRILI



### Maisha Yako Ya Nyuma Yanakuzuia?

Na Jeff Bates

Kijana mkubwa anashiriki jinsi kumwali-ka Yesu Kristo katika maisha yetu kuna-yoweza kutusaidia kusonga mbele.



### Kutumia Jina Kamili la Kanisa Ilikuwa Vigumu lakini Ilistahili Na Lauri Ahola

Kijana mkubwa anashiriki jinsi kufuata ushauri wa Rais Nelson kulivyomuwezesha kushiriki injili vizuri zaidi.



### Kupata Furaha katika Kufanya Kazi ya Bwana

Vijana wakubwa kote ulimwenguni wana-shiriki jinsi ambavyo wanachangia katika Urejesho unaoendelea.

## TAFUTA ZAIDI

Kwenye Gospel Library app na kwenye liahona.ChurchofJesusChrist.org, unaweza:

- Kupata toleo la sasa.
- Kugundua yaliyomo-ya kidijitali pekee.
- Kutafuta matoleo yaliyopita.
- Kuwasilisha hadithi na majibu yako.
- Kuagiza au kutoa agizo la zawadi.
- Kuzidisha usomaji kwa vifaa vya kidijitali.
- Kushiriki makala na video unazozipenda sana.
- Kupakua au kuchapisha makala.
- Kusikiliza makala zako uzipendazo.

## WASILIANA NASI

Tuma maswali na majibu yako kwenda liahona@ChurchofJesusChrist.org.

Wasilisha hadithi zako nenda kwenye liahona.ChurchofJesusChrist.org au tuma barua kwenda:

Liahona, floor 23

50 East North Temple Street

Salt Lake City, UT 84150-0023, USA

#### APRILI 2020 VOL. 7 NO. 1 LIAHONA 16719 743

Gazeti la Kimataifa la Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

**Urais wa Kwanza:** Russell M. Nelson, Dallin H. Oaks, Henry B. Eyring

**Akidi ya Mitume Kumi na Wawili:** M. Russell Ballard, Jeffrey R. Holland, Dieter F. Uchtdorf, David A. Bednar, Quentin L. Cook, D. Todd Christofferson, Neil L. Andersen, Ronald A. Rasband, Gary E. Stevenson, Dale G. Renlund, Gerrit W. Gong, Ulisses Soares

**Mhariri:** Randy D. Funk

**Washauri:** Becky Craven, Sharon Eubank, Cristina B. Franco, Walter F. González, Larry S. Kacher, Jan E. Newman, Adrián Ochoa, Michael T. Ringwood, Vern P. Stanfill

**Mkurugenzi Mtendaji:** Richard I. Heaton

**Mkurugenzi wa Magazeti ya Kanisa:** Allan R. Loyborg

**Meneja wa Biashara:** Garff Cannon

**Mhariri Mtendaji:** Adam C. Olson

**Mhariri Mtendaji Msaidizi:** Ryan Carr

**Mchapishaji Msaidizi:** Camila Castrillón

**Kuandika na kuhariri:** David Dickson, David A. Edwards, Matthew D. Flitton, Garrett H. Garff, Jon Ryan Jensen, Aaron Johnston, Charlotte Larcabal, Michael R. Morris, Eric B. Murdock, Joshua J. Perkey, Jan Pinborough, Richard M. Romney, Mindy Selu, Lori Fuller Sosa, Marissa Widdison

**Mkurugenzi wa Sanaa:** Tadd R. Peterson

**Usanifu:** Jeanette Andrews, Fay P. Andrus, Mandie Bentley, C. Kimball Bott, Thomas Child, Joshua Dennis, David Green, Colleen Hinckley, Eric P. Johnson, Susan Lofgren, Scott M. Mooy, Aleni Regehr, Mark W. Robison, K. Nicole Walkenhorst

**Mratibu wa Haki Miliki:** Collette Nebeker Aune

**Meneja wa Uzalishaji:** Jane Ann Peters

**Uzalishaji:** Ira Glen Adair, Julie Burdett, José Chavez, Thomas G. Cronin, Bryan W. Gygi, Ginny J. Nilson, Marrison M. Smith

**Kabla ya Chapa:** Joshua Dennis, Amnon Harris

**Mkurugenzi wa Uchapishaji:** Steven T. Lewis

**Mkurugenzi wa Usambazaji:** Nelson Gonzalez

Kwa usajili na bei nje ya Marekani na Kanada, nenda kwenye store. ChurchofJesusChrist.org au wasiliana na kituo cha usambazaji cha Kanisa katika eneo lako ama kiongozi wa kata au wizi.

Wasilisha miswada na maswali katika liahona.ChurchofJesusChrist.org; na barua pepe liahona.ChurchofJesusChrist.org; ama kwa barua Liahona, Rm. 2420, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150-0024, USA.

*Liahona* (neno katika Kitabu cha Mormoni linaloanishwa "dira" ama "kielekezi") imechapishwa katika Kiabeni, Kiarmeni, Bislama, Kibulgaria, Kikambodia, Kisebuano, Kichina, Kichina (kiiichorahisishwa), Kikroesia, Kicheki, Kidenishi, Kiholanzi, Kiingereza, Kiestoni, Kifiji, Kifinishi, Kifaransa, Kijerumani, Kigiriki, Kiangaria, Kaislandi, Kiindonesia, Kiitaliano, Kijapani, Kikiribati, Kikorea, Kilatvia, Kiliithuania, Kimalagasi,

Kimarshalizi, Kimongolia, Kinorwei, Kipolishi, Kireno, Kiromania, Kirusi, Kisamoa, Kislovenia, Kihispania, Kiswahili, Kiswidi, Kitagalogi, Kitahiti, Kithai, Kitonga, Kiukreni, Kiurdu, na Kivietinamu. (Masafa hutofautiana kwa lugha.)


© 2020 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa Limepigwa chapa Marekani.

**Taarifa ya Hakimiliki:** Isipokuwa imeelezwa vinginevyo, watu binafsi wanaweza kunakili yaliyomo katika Liahona hii kwa matumizi yao binafsi, yasiyo ya kibiasara (ikijumuisha kwa miito ya Kanisa). Haki hiyo yaweza kuondolewa wakati wa wote. Kazi za picha zisinakiliwe kama kuna zuio linaloeleza hivyo kwenye mstari pembeni ya mchoro. Maswali juu ya hakimiliki yaelekezwe kwa Intellectual Property Office, 50 E. North Temple St., FL 13, Salt Lake City, UT 84150, USA; email: cor-intellectualproperty@ChurchofJesusChrist.org.

**For Readers in the United States and Canada:** April 2020 Vol. 7 No. 1.

LIAHONA (USPS 311-480) Swahili (ISSN 2326-3695) is published twice a year (April and October) by The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150. USA subscription price is \$1.00 per year; Canada, \$1.20 plus applicable taxes. Periodicals Postage Paid at Salt Lake City, Utah. Sixty days' notice required for change of address. Include address label from a recent issue; old and new address must be included. Send USA and Canadian subscriptions to Salt Lake Distribution Center at address below. Subscription help line: 1-800-537-5971. Credit card orders (American Express, Discover, MasterCard, Visa) may be taken by phone or at store.ChurchofJesusChrist.org. (Canada Post Information: Publication Agreement #40017431)

POSTMASTER: Send all UAA to CFS (see DMM 507.1.5.2). NONPOSTAL AND MILITARY FACILITIES: Send address changes to Distribution Services, Church Magazines, P.O. Box 26368, Salt Lake City, UT 84126-0368, USA.



## MKUTANO MKUU MIAKA YOTE

Sasa katika mwaka wake wa 190, mkutano mkuu ni desturi ya kudumu kila Aprili na Oktoba, lakini kumekuwa na mabadiliko ya kupendeza katika miaka iliyopita:



### 1830

Miezi miwili baada ya Kanisa kuanzishwa, Joseph Smith alisimamia mkutano mkuu wa kwanza kule Fayette, New York. Takribani waumini 30 na wengine kadhaa walihudhuria.

### 1850

*Deseret News* ilichapisha ripoti ya kwanza kamili ya mkutano kwa sababu mwanahabari kijana, George D. Watt, alikuwa ameweza kuandika muhtasari wa hotuba kwa kifupi.

### 1867

Mkutano mkuu ulidumu kwa muda wa siku nne badala ya siku tatu kama kawaida kwa sababu mkusanyiko ulipiga kura kuendelea kuwepo kwa siku moja zaidi.

### 1924

Mikrofoni zilitumika kwa mara ya kwanza kwenye mimbari ndani ya Tabernako. Awali, wanenaji walitegemea nguvu ya sauti zao ili waweze kusikika.

### 1949

Kwa kutumia kamera ndani ya Tabernako, mkutano kwa mara ya kwanza ulioneshwa kwenye televisheni.

two P. M. Conference called to order by W. Snow; singing, prayer by W. Snow, singing. Elder O. Hyde delivered a lecture to the Honorable Chancellor and board of Regents of the University of the State of Deseret, in presence of the Conference, on Education. Education is not confined to letters only, but to the excluding of all darkness, and when a man has ascended to the summit, he

guage is better than n If you could bring all thers now living, tog will express their ideat words, and they wil that our language is yet we have to use th have, in order to acco object which is before fil the obligations we one to the other, by u struments already in o A certain portion of perty ought to be det



### 1962

Hotuba zilifasiriwa katika lugha tofauti—Kijerumani, Kiholanzi, na Kihispania—kwa mara ya kwanza ndani ya Tabernako. Sasa hotuba zinafasiriwa katika zaidi ya lugha 90!

### 1967

Mkutano mkuu ulioneshwa kwenye TV kwa rangi. Wanaume wa Kwaya ya Tabernako walivalia makoti ya rangi ya samawati, na wanawake wakavalia blauzi za rangi ya salmoni.

### 1977

Ukibadilika kutoka siku tatu na vikao sita vikuu, mkutano ulichukua muda wa siku mbili na kujumuishia vikao vitano vikuu.

### 2000

Kituo kipya cha Mikutano Jijini Salt Lake, chenye uwezo wa kuchukua idadi ya watu 21,000 walioketi, kilikuwa mwenyeji wa mkutano mkuu kwa mara ya kwanza.

Kupata mahubiri kutoka mikutano mkuu ya sasa na iliyopita, tembelea [gc.Church of Jesus Christ.org](http://gc.ChurchofJesusChrist.org) au sehemu ya “Mkutano Mkuu” ya app ya Maktaba ya Injili.






---

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho linauandaa ulimwengu kwa ajili ya siku ambayo “dunia itajawa na kumjua Bwana” (Isaya 11:9).





Na Rais  
Russell M. Nelson

# Siku za Baadaye za Kanisa

## KUUANDAA ULIMWENGU KWA AJILI YA UJIO WA PILI WA MWOKOZI

**M**imi na wewe tunayo nafasi ya kushiriki katika Urejesho unaoendelea wa injili ya Yesu Kristo. Ni ajabu! Haijate-ngenezwa na mtu. Inakuja kutoka kwa Bwana, ambaye alisema, “Nitaiharakisha kazi yangu katika wakati wake” (Mafundisho na Maagano 88:73). Kazi hii inahalalishwa na tangazo takatifu lililotolewa miaka 200 iliyopita. Ilikuwa na maneno sita pekee: “Huyu ni Mwanangu Mpendwa. Msikilize Yeye!” (Ona Historia ya—Joseph Smith 1:17).

Iikitamkwa na Mwenyezi Mungu, tangazo hilo lilimleta mvulana Joseph Smith kwa Bwana Yesu Kristo. Hayo maneno sita yalianzisha Urejesho wa injili Yake. Kwa nini? Kwa sababu Mungu wetu aliye hai ni Mungu wa upe-ndo! Anawataka watoto Wake wapate kutokufa na uzima wa milele! Kazi kuu ya siku za mwisho ambayo sisi ni sehemu yake ilianzishwa, kwa wakati, kubariki ulimwengu uliokuwa unasubiri na kulia.

Siwezi kuzungumzia Urejesho kimya kimya. Ukweli huu wa historia hakika ni mzuri mno! Ni wa ajabu! Ni wa kustaajabisha! Ni ajabu gani kwamba malaika kutoka mbinguni walikuja kutoa mamlaka na nguvu kwa ajili ya kazi hii?

Leo, kazi ya Bwana katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho inasonga mbele kwa kasi mno. Kanisa litakuwa na siku za baadaye ambazo hazijashuhudiwa, zisizo za kufanananishwa. “Jicho hali-kuyaona, wala sikio halikuyasikia, . . . mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao” (1 Wakorintho 2:9; ona pia Mafundisho na Maagano 76:10).

Kumbuka kwamba utimilifu wa huduma ya Kristo upo katika siku za baadaye. Unabii wa Ujio Wake wa Pili haujatimizwa. Tunajiandaa tu kufikia kilele cha kipindi hiki cha mwisho—wakati Ujio wa Pili wa Mwokozi utakuwa uhalisia.

### **Kukusanya Israeli kutoka Pande Zote Mbili za Pazia.**

Kitendo muhimu cha kutangulia Ujio huo wa Pili ni kukusanywa kwa Israeli kulikosubiriwa kwa muda mrefu (ona 1 Nefi 15:18; ona pia ukurasa wa jina wa Kitabu cha Mormoni). Mafundisho haya ya ukusanyaji ni mojawapo ya mafunzo muhimu ya Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Bwana ametangaza: Ninawapatia ishara . . . kwamba nitawakusanya ndani, baada ya kutawanyika kwa muda mrefu, watu wangu, Ee nyumba ya Israeli, na nitaanzisha tena miongoni mwao Sayuni yangu” (3 Nefi 21:1).

Hatufundishi tu kanuni hii, lakini tunaishiriki pia. Tunafanya hivyo tunaposaidia kuwakusanya

wateule wa Bwana kutoka pande zote mbili za pazia. Kama sehemu ya takdiri iliyopangwa kwa ajili ya dunia na wakazi wake, jamaa zetu walioaga dunia wanahitaji kukombolewa (ona Mafundisho na Maagano 128:15). Kwa huruma, mwaliko wa “kuja kwa Kristo” (Yakobo 1:7; Moroni 10:32; Mafundisho na Maagano 20:59) unaweza pia kutolewa kwa wale waliofariki bila ufahamu wa injili (ona Mafundisho na Maagano 137:6–8). Sehemu ya matayarisho yao, hata hivyo, inahitaji juhudi za wengine duniani. Tunakusanya chati za ukoo, tunatengeneza shiti za vikundi vya familia, na kufanya kazi ya hekalu kwa niaba ili kukusanya watu kwa Bwana na katika familia zao (ona 1 Wakorintho 15:29; 1 Petro 4:6).

Familia zinahitaji kuunganishwa pamoja milele (ona Mafundisho na Maagano 2:2–3; 49:17; 138:48; Historia ya—Joseph Smith 1:39). Muunganiko wa kuweka pamoja unapaswa kuwekwa baina ya akina baba na watoto. Katika wakati wetu, muungano wote, mkamilifu, na ulio kamili wa vipindi vyote, funguo, na

*Kumbuka  
kwamba utimilifu  
wa huduma ya  
Kristo upo katika  
siku za baadaye.*





nguvu vinapaswa kuunganishwa pamoja (ona Mafundisho na Maagano 128:18). Kwa ajili ya malengo haya matakatifu, mahekalu matakatifu sasa yanapatikana kote ulimwenguni. Ninasisitiza tena ya kwamba ujenzi wa mahekalu haya huenda usibadilisha maisha yenu, lakini huduma yenu hekaluni hakika itabadilisha.

Wakati unakuja ambapo wale wasiomtii Bwana watatengwa na wale wanaomtii (ona Mafundisho na Maagano 86:1–7). Bima yetu salama kabisa ni kuendelea kuwa wastahiki wa kukubaliwa kuingia katika nyumba Yake takatifu. Zawadi kubwa ambayo unaweza kumpa Mungu ni kujilinda kutokana na mawaa kutoka kwenye ulimwengu, mstahiki kuabudu katika nyumba Yake takatifu. Zawadi Yake kwako itakuwa amani na usalama wa kujua kwamba wewe ni mstahiki wa kukutana na Naye, wakati wowote siku hiyo itakapofika.

Kando na kazi ya hekaluni, kuja kwa Kitabu cha Mormoni ni ishara kwa ulimwengu mzima

kwamba Bwana ameanza kukusanya Israeli na kutimiza maagano Aliyofanya na Ibrahimu, Isaka, na Yakobo (ona Mwanzo 12:2–3; 3 Nefi 21; 29). Kitabu cha Mormoni kinatangaza mafundisho ya kukusanya (ona, kwa mfano, 1 Nefi 10:14). Kinasababisha watu kujifunza kuhusu Yesu Kristo, kuamini injili Yake, na kujiunga na Kanisa Lake. Kwa kweli, kama kusungekuwa na Kitabu cha Mormoni, mkusanyiko ulioahidiwa wa Israeli haungetokea.

Kazi ya umisionari pia ni muhimu katika kukusanya huko. Watumishi wa Bwana husonga mbele wakihubiri Urejesho. Katika mataifa mengi waumini na wamisionari wetu wamewatafuta wale ambao ni Israeli iliyo-tawanyika; wamewawinda kutoka kwenye “pango za majabali” (Yeremia 16:16); na wamewavua, kama katika siku za kale.

Kazi ya umisionari inawaunganisha watu kwenye agano Bwana alilofanya na Ibrahimu zamani:

“Nawe utakuwa baraka kwa uzao wako baada yako, ili katika mikono yao wataichukua huduma hii na Ukuhani kwa mataifa yote;

“Nami nitawabariki wao kupitia jina lako; kwani kadiri wengi watakavyoipokea Injili hii wataitwa kwa jina lako, nao watahesabiwa kuwa uzao wako, na watainuka na kukubariki, kama baba yao” (Ibrahimu 2:9–10).

Kazi ya umisionari ni mwanzo tu wa baraka hiyo. Kutimizwa, kukamilishwa, kwa baraka hizo huja wakati ambapo wale ambao wameingia katika maji ya ubatizo wanakamilisha maisha yao kufikia kiasi cha wao kuingia katika hekalu takatifu. Kupokea endaumenti huko kunawaunganisha waumini wa Kanisa katika agano la Ibrahimu.

Uamuzi wa kuja kwa Kristo si suala la kieneo; ni suala la kujitolea kwa mtu binafsi. Waumini wote wa Kanisa wanaweza kupata mafundisho, ibada, funguo za ukuhani, na baraka za injili, bila kujali eneo lao. Watu wanaweza “kuletwa kwenye ufahamu wa maarifa ya Bwana” (3 Nefi 20:13) bila ya kuondoka kwenye ardhi zao za nyumbani.

Kweli, katika siku za mwanzo za Kanisa, uongofu kawaida ulimaanisha uhamiaji pia. Lakini sasa kukusanyika kunafanyika katika kila taifa. Bwana ametangaza kujengwa kwa Sayuni (ona Mafundisho na Maagano 6:6; 11:6) katika kila ufalme ambapo Amewapa Watakatifu Wake uzao wao na utaifa. “Mahali pa kukusanyika kwa Watakatifu wa Brazili ni Brazili; mahali pa kukusanyika kwa Watakatifu wa Nigeria ni Nigeria; mahali pa

---

*Zawadi kubwa ambayo unaweza kumpa Bwana ni kujilinda kutokana na mawaa kutoka kwenye ulimwengu, mstahiki kuabudu katika nyumba Yake takatifu.*



*Ninawaahidi ya kwamba mnapomfuata Yesu Kristo, mtapata amani ya kudumu na furaha ya kweli.*

kukusanyika kwa Watakatifu wa Korea ni Korea. Sayuni ni “walio safi moyoni” (Mafundisho na Maagano 97:21). Ni popote walipo Watakatifu wenye haki.

Usalama wa kiroho daima utategemea *jinsi* mtu anavyoishi, si *pahali* mtu anapoishi. Ninaahidi ya kwamba kama tutafanya kadri ya uwezo wetu kuwa na imani katika Yesu Kristo na kufikia uwezo wa Upatanisho Wake kupitia toba, tutapata uelewa na nguvu za Mungu kutusaidia kupeleka baraka za injili ya urejesho ya Yesu Kristo katika kila taifa, ukoo, ndimi, na watu na kuuandaa ulimwengu kwa Ujio wa Pili wa Bwana.

### **Ujio wa Pili**

Bwana atarudi kwenye ile nchi ambayo Aliifanya kuwa takatifu kupitia misheni Yake huko katika maisha ya kufa. Kwa shangwe, Atarudi tena Yerusalemu. Akiwa amevalia mavazi ya rangi nyekundu ambayo yanaashiria damu yake, ambayo ilivuja kutoka kwenye kila kinyweleo, Atarudi kwenye lile Jiji Takatifu (ona Mafundisho na Maagano 133:46–48). Huko na

kwingineko, “utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja” (Isaya 40:5; ona pia Mafundisho na Maagano 101:23). “Jina lake litaitwa, Ajabu, Mshauri, Mwenyezi Mungu, Baba asiye na mwisho, Mwana Mfalme wa Amani” (Isaya 9:6).

Atatawala kutoka miji miwili mikuu ya dunia: mmoja katika Yerusalemu ya kale (ona Zakaria 14) na mwingine katika Yerusalemu Mpya “iliyojengwa juu ya bara la Amerika” (Makala ya Imani 1:10). Kutoka vituo hivi Ataendesha mambo ya Kanisa na Ufalme Wake. Hekalu lingine kisha litajengwa Yerusalemu. Kutoka katika hekalu hilo Atatawala milele kama Bwana wa Mabwana. Maji yatatoka chini ya hekalu. Maji ya Bahari ya Chumvi yataponywa. (Ona Ezekieli 47:1–8.)

Katika siku hiyo Yeye atamiliki majina mapya na kuzungukwa na Watakatifu maalum. Atajulikana kama “Bwana wa Mabwana, na Mfalme wa Wafalme, na hao ambao [watakuwa] pamoja naye [watakuwa ni wale] walioitwa, na wateule, na waaminifu” (Ufunuo 17:14) kwa kuamini kwao

katika maisha ya sasa. Kisha “atawala milele na milele” (Ufunuo 11:15).

Dunia itarejeshwa katika hali yake ya kiparadiso na kufanywa kuwa mpya. Kutakuwa na mbingu mpya na nchi mpya (ona Ufunuo 21:1; Etheri 13:9; Mafundisho na Maagano 29:23–24).

Ni jukumu letu—ni heshima yetu—kusaidia kuandaa ulimwengu kwa ajili ya siku hiyo.

### **Kabiliana na Siku za Baadaye kwa Imani**

Kwa sasa, hapa na kwa wakati huu, tunaishi katika muda wa matatizo. Matetemeko ya ardhi na tsunami husababisha maafa, serikali zina-vunjika, matatizo ya uchumi ni makali, familia inashambuliwa, na viwango vya talaka vinao-gezeke. Tuna sababu kuu za kuwa na wasiwasi. Lakini hatuhitaji kuruhusu hofu yetu ichukue nafasi ya imani yetu. Tunaweza kukabiliana na hofu hizo kwa kuimarisha imani yetu.

Kwa nini tunahitaji imani thabiti kama hiyo? Kwa sababu ya siku ngumu zilizo mbele. Ni nadra katika siku za baadaye kuwa rahisi au ya kupendeza kuwa Mtakatifu wa Siku za Mwisho mwaminifu. Kila mmoja wetu atajaribiwa. Mtume Paulo alionya kuwa katika siku za mwisho, wale wanaomfuata Bwana kwa bidii “watapata mateso” (2 Timotheo 3:12). Mateso hayo hayo yanaweza ama kukuvunja hata kwenye udhaifu kimya au kukutia motisha wewe kuwa mfano mwema na kuwa jasiri katika maisha yako ya kila siku.

*Jinsi* unavyokabiliana na majaribu ya maisha ni sehemu ya ukuaji wa imani yako. Nguvu huja wakati wewe unapokumbuka kwamba wewe una asili takatifu, urithi wa thamani usio na kipimo. Bwana amekukumbusha, watoto wako, na waju-kuu wako kwamba nyinyi ni warithi kisheria, kwamba mmehifadhiwa mbinguni kwa muda na wakati wenu maalum wa kuzaliwa, kukua na kuwa wapeperushaji wa bendera Yake na watu Wake wa agano. Unapoingia katika njia ya Bwana ya haki, utabarikiwa kuendelea katika wema

Wake na kuwa nuru na mwokozi kwa watu Wake (ona Mafundisho na Maagano 86:8–11).

Fanya kila uwezalo kuimarisha imani yako katika Yesu Kristo kwa kuzidisha uelewa wako wa mafundisho yanayofundishwa katika Kanisa Lake lililorejeshwa na kwa kutafuta ukweli bila kutulia. Ukiweka nanga kwenye mafundisho safi, utaweza kusonga mbele kwa imani na msimamo thabiti na kwa furaha kufanya kadri ya uwezo wako wote kutimiza malengo ya Bwana.

Kutakuwa na siku ambapo utavunjika moyo. Kwa hivyo sali kwa ajili ya ujasiri wa kutokata tamaa! Kwa huzuni, baadhi ya wale uliowadhania kuwa marafiki watakusaliti. Na baadhi ya vitu vitaonekana tu kuwa haviko sawa.

Hata hivyo, ninawaahidi ya kwamba mnapomfuata Yesu Kristo, mta-pata amani ya kudumu na furaha ya kweli. Unaposhika maagano yako kwa ongezeko la usahihi, na unapolinda Kanisa na ufalme wa Mungu duniani leo, Bwana atakubariki kwa nguvu na busara ya kutimiza kile ambacho ni waumini tu wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho wanaweza kutimiza.

Tunapaswa kuwa waje-nzi wa imani binafsi kati-ka Mungu, imani katika Bwana Yesu Kristo na imani katika Kanisa Lake. Tunapaswa kujenga familia na kuunganishwa katika mahekalu matakatifu. Tunapaswa kujenga Kanisa na ufalme wa Mungu hapa duniani (ona Mathayo 6:33). Tunapaswa kujita-yarisha kwa ajili ya takdiri yetu takatifu: utukufu, kutokufa, na uzima wa milele (ona Warumi 2:7; Mafundisho na Maagano 75:5).

Ninashuhudia kwa unyenyekevu kwenu kwamba—kama alivyotangaza Nabii Joseph Smith—injili ya Yesu Kristo iliyorejeshwa “itasonga mbele kwa ujasiri, uadilifu, na kwa uhuru, hadi itakapoingia kila bara, kutembe-lea kila tabia ya nchi, kufagia kila nchi, na kusikika katika kila sikio, hadi pale malengo la Mungu yatakapokamilika, na Yehova Mkuu atakapose-ma kazi imekwisha” (*Historia ya Kanisa*, 4:540).

Tumejiingiza katika kazi ya Mwenyezi Mungu. Ninasali kwamba bara-ka Zake ziwe pamoja na kila mmoja wenu. ■

---

*Nguvu huja wakati wewe  
unapokumbuka kwamba wewe  
una asili takatifu, urithi wa  
thamani usio na kipimo.*



## Berglind Guðnason

Árnessýsla, Iceland



*Berglind (kushoto) pamoja na dada yake Elín (kulia). Wakati Berglind alipokumbana na mfadhaiko mkubwa zaidi ambao amewahi kupitia, alihisi kwamba hangeweza kuendelea. Kwa kuzungumzia mapambano yake pamoja na familia na marafiki, amepata uponyaji wa kiroho na kihisia kupitia vifaa ambavyo Baba wa Mbinguni ametoa.*

**MINDY SELU, MPIGA PICHA**

Kuzungumza kuhusu mfadhaiko wangu pamoja na familia na marafiki kumenisaidia sana. Pia ilileta usaidizi zaidi. Sikutaka kumeza vidonge au kwenda kwenye matibabu. Nilishinda nikijiambia, "Niko na Mungu." Lakini Mungu anatoa vifaa vingine vingi, kama vile madawa na matibabu, kwa matumizi yetu ikiwa ni pamoja na vitu vya kiroho.

Wakati nilipokuwa katika mfadhaiko wangu mbaya zaidi, watu wangeniambia, "Itakuwa sawa." Ningechoka sana kusikia hivyo lakini, ajabu na inavyosikika, ni kweli.

Sikuwahi kufikiria ningekuwa na furaha kama vile nilivyo sasa. Siku zingine bado napambana, lakini pamoja na vifaa ambavyo Baba wa Mbinguni amenipa mimi, naweza kufanikiwa. Sasa wakati nahisi nikiteleza katika mfadhaiko, ninajiambia ninapendwa, ninao watu wa kuzungumza nao, na mambo yatakuwa sawa.

### GUNDUA ZAIDI

Ona mengi kuhusu safari ya imani ya Berglind, ikijumuisha picha za ziada, kwenye toleo la mtandaoni au Maktaba ya Injili ya makala hii kwenye [ChurchofJesusChrist.org/go/42013](https://ChurchofJesusChrist.org/go/42013).

# Kanuni za Kuhudumu

## KUHUDUMU KUPITIA MKUTANO MKUU

*Pamoja na dondoo zote za kuinua, desturi za familia, na mafundisho kutoka kwa watumishi wa Bwana, mkutano mkuu unatupatia njia nyingi za kuhudumu—kabla, wakati wa, na baada ya wikiendi ya mkutano mkuu!*

**K**ama walimu wa darasa la matayarisho ya misheni, Susie na Tom Mullen kawaida wao huwapa washiriki wa darasa lao changamoto ya kumwalika mtu fulani kutazama mkutano mkuu pamoja nao.

“Kumwalika mtu kufanya jambo fulani ni sehemu muhimu ya kazi ya umisionari, na inatumika kwenye kuhudumu pia,” anasema. “Wanafunzi wetu hutoa ripoti mara kwa mara kuhusu jinsi ilivyofanyika vyema kwao na pia mtu ambaye walimualika.”

Hapa ni njia chache ambazo wanafunzi wao waliripoti kuhusu kufikia:

- “Sisi humhudumia rafiki ambaye ana shida fulani anazopambana nazo. Tuli-mualika asikilize mkutano mkuu kwa ajili ya majibu. Wakati tulipomtembelea baada ya mkutano mkuu, alituelezea kwamba alisikia mawazo mengi ambayo yangemsaidia.”
- “Tulifanya sherehe ya mkutano mkuu na kila mtu alileta asusa za kushiriki. Iliku-wa furaha kubwa kwamba tuliamua kufanya hivyo tena.”
- “Nlimualika rafiki atazame mkutano mkuu pamoja nami. Tulipokuwa tukizungu-mza kuhusu mkutano mkuu, tuliamua kusafiri kwa gari hadi kwenye jumba la mikutano kuona kama tungeweza kuutazama kutokea pale. Tuliweza, na ilikuwa uzoefu mzuri zaidi kuwa pale!”

Jinsi akina Mullen na wanafunzi wao walivyojifunza, kuna njia nyingi za kuhudumu kupitia mkutano mkuu. Ni njia nzuri ya kushiriki dondoo za kuinua, desturi za familia, mijadala ya maana, na mafundisho ya watumishi wa Bwana!







## KANUNI ZA KUZINGATIA

### “Tambua”

Mwokozi kwa upendo alitumia muda kuona mahitaji ya wengine kisha akashughulikia mahitaji hayo (ona Mathayo 9:35–36; Yohana 6:5; 19:26–27). Tunaweza kufanya vivyo hivyo.

### “Alika mara moja”

Baada ya kutambua mahitaji ya wale tunao-wahudumia, hatua inayofuata ni kutenda.

### “Kusikia maneno ya manabii”

Ni sharti “kukutana pamoja mara kwa mara” (Moroni 6:5) kujifunza pamoja, kukua pamoja, na kuzungumza kuhusu vitu vya kiroho ambavyo ni vya muhimu zaidi kwa nafsi zetu. “Njoo, usikie sauti ya nabii, na usikie neno la Mungu”<sup>2</sup> unaweza kuwa mwaliko muhimu zaidi tunaowapa wale tunaowahudumia.

### “Upendo na urafiki”

Ili kuwasaidia na kuwashawishi wengine kwa kweli, ni lazima tujenge mahusiano ya huruma na “upendo usio unafiki” (ona Mafundisho na Maagano 121:41).

## Alika Wengine Nyumbani Kwako.

*“Mwokozi alitwaamuru wafuasi Wake ‘mpendane, kama nilivyowapenda ninyi’ (Yohana 13:34). Kwa hivyo tunaangalia jinsi Alivyotupenda. . . . Kama tutamchukua Yeye kuwa mfano wetu, ni sharti siku zote tujaribu kumjumuisha kila mtu.” —Rais Dallin H. Oaks<sup>1</sup>*

Miaka mingi iliyopita mwalimu wetu wa nyumbani Mike **ali-gundua** kwamba mimi na watoto wangu watatu tulikuwa na kompyuta ndogo ya kutazama mkutano mkuu. **Mara moja alitualika** kwenda nyumbani kwake kutazama pamoja naye na mkewe, Jackie, akisisitiza kwamba tungefurahia wenza wao. Watoto wangu walifurahia kutazama mkutano kwenye TV ya kweli; nilifurahia pakubwa kupata msaada huo; na tulifurahia wakati wetu pamoja.

Baada ya hapo, kutazama mkutano mkuu pamoja ilikuwa des-turi. Hata baada ya kupata TV yetu, kwa furaha bado tulienda kwa Mike na Jackie na mito yetu, madaftari, na asusa kwa ajili ya mku-tano mkuu. **Kusikia maneno ya manabii** pamoja iliufanya kuwa maalum. Tulikuwa kama familia. Mike na Jackie walikuja kuwa baadhi ya rafiki zangu wazuri zaidi na mababu wa pili kwa watoto wangu. **Upendo na urafiki** wao umekuwa baraka ya ajabu kwa familia yangu. Nina shukrani kwa ajili ya utayari wao kufungua nyumba yao na mioyo yao kwetu.

**Suzanne Erd, California, Marekani**

## Shiriki kwenye mtandao

*“Mitandao ya kijamii ni vifaa vya kimataifa ambavyo vinaweza kibinafsi na kwa njia chanya kuathiri idadi kubwa ya watu binafsi na familia. Ninaamini wakati umefika kwetu kama wafuasi wa Kristo kutumia zana hizi zenye ushawishi kwa usahihi na kwa weledi zaidi kushuhudia juu ya Mungu Baba wa Milele, mpango Wake wa furaha kwa watoto Wake, na Mwanawe, Yesu Kristo, kama Mwokozi wa ulimwengu.”*  
—Mzee David A. Bednar<sup>3</sup>

Wavuti inaturuhusu **kushiriki injili** pamoja na ulimwengu mzi-ma. Ninalipenda hilo! Hii inajumuisha sehemu ya mkutano mkuu ambapo mimi hushiriki shughuli chache kwa ajili ya mkutano mkuu, lakini sana sana mimi hujaribu kuwasaidia wengine **kubuni mjadala** kutoka kwenye hotuba za mkutano mkuu. Kuona maswali kutoka kwa wengine kawaida kunaweza kutusaidia kuona vitu kwa mtazamo mpya na inaweza kuwa ubao wa kutupia maswali yetu makuu ya mjadala.

Nimegundua kwamba **unapotumia maswali** kujadili hotuba za mkutano mkuu pamoja na familia unazozihudumia, hilo linakusaidia kuona nguvu yao na vile vile mahitaji yao. Mojawapo ya maswali ninayopenda kuuliza ni, Unahisi nini ilikuwa dhamira kutoka kwenye kikao cha hivi karibuni cha mkutano mkuu?

Jibu karibu kila wakati linakuwezesha kuona kile kinachoendelea katika maisha yao na kile ambacho ni muhimu kwao. Inatoa nafasi kwako kuwa kaka au dada bora mhudumiaji kwa sababu unapata nafasi ya kuwaona kwa uwazi zaidi. ■

Camille Gillham, Colorado, Marekani

### MUHTASARI

1. Dallin H. Oaks, “Upendo na Sheria” (video), mormonandgay.ChurchofJesusChrist.org.
2. “Come, Listen to a Prophet’s Voice,” *Nyimbo za Kanisa*, na. 21.
3. David A. Bednar, “Kujaza Dunia kupitia Mitandao ya Kijamii,” *Liahona*, Ago. 2015, 50.
4. *Hubiri Injili Yangu: Mwongozo wa Huduma ya Umisionari* (2004), 185.

## KANUNI ZA KUZINGATIA

### “Shiriki injili”

Tumeweka agano “kusimama kama mashahidi wa Mungu nyakati zote, na katika vitu vyote na katika mahali popote” (Mosia 18:9).

### “Buni mjadala”

Jumbe za mkutano mkuu zinaweza kutia msukumo wa mazungumzo, mazuri, yanayofaa, na yanayoongozwa kiroho. Na mijadala ya aina hii inaweza kuimarisha mahusiano, kusaidia ushuhuda kukua, na kukuletea furaha! (ona Mafundisho na Maagano 50:22).

### “Tumia maswali”

“Maswali mazuri yatakusaidia kuelewa mapeleleleo, wasiwasi, au maswali ambayo wengine wanayo. Yanaweza kuboresha kufundisha kwako, kualika Roho, na kuwasaidia watu kujifunza.”<sup>4</sup>





**Na Mzee  
LeGrand R. Curtis Jr.**

Kiongozi Mkuu  
Mwenye Mamlaka  
wa Sabini na  
Mwanahistoria  
wa Kanisa na  
Mwandishi wa  
Kumbukumbu

# UREJESH



---

Urejesho ulianza katika Msitu  
Mtakatifu miaka 200 iliyopita  
na unaendelea leo—na mimi  
na wewe tunaweza kuwa  
sehemu yake.



# O Unaoendelea

**H**uu ni wakati wa kupendeza na kusisimua kuwa ulimwenguni. Tumebarikiwa kushiriki katika matukio makuu yanayofanyika katika kipindi cha utimilifu wa nyakati, kama matayarisho kabla ya Ujio wa Pili wa Bwana.<sup>1</sup> Tuna nafasi si tu ya kushuhudia matukio haya ya ajabu yakijitokeza lakini pia kuwa sehemu yake.<sup>2</sup>

Wakati mwingine tunazungumzia Urejesho wa injili kana kwamba ulifanyika kwa wakati mmoja. Miaka mia mbili iliyopita, Ono la Kwanza lilianzisha mchakato, lakini Urejesho kamwe, bila shaka, haukuishia hapo. Kazi ya Bwana kupitia Joseph Smith na washiriki wake iliendelea kwa kutafsiri Kitabu cha Mormoni, kurejeshwa ukuhani, kuanzisha Kanisa, kuwatumia wamisionari, kujenga mahekalu, kuanzisha Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama, na

kadhalika. Matukio haya ya Urejesho yalianza mnamo mwaka 1820 na kuendelea maisha yote ya Joseph Smith.

Ajabu ilivyo vitu ambavyo Mungu alifunua kupitia kwa Joseph Smith, Urejesho haukukamilika katika maisha ya Joseph. Kupitia manabii waliomfuata tumepokea vitu kama ukuaji unaoendelea wa kazi ya hekaluni; maandiko ya ziada; kutafsiriwa kwa maandiko katika lugha mbalimbali; kuenezwa kwa injili kote ulimwenguni; kuanzishwa kwa Shule ya Jumapili, Wasichana, Msingi, na akidi za ukuhani; na marekebisho mengi ya mpangilio na utaratibu wa Kanisa.

“Sisi ni mashahidi wa mchakato wa urejesho,” Rais Russell M. Nelson amesema. “Kama unadhani Kanisa limerejeshwa kikamilifu, unashuhudia mwanzo tu. Kuna mengi zaidi yanakuja. . . . Subiri hadi mwaka ujao. Na kisha mwaka

*Mungu ametupa-  
tia nafasi nzuri  
kabisa ya kutekele-  
za wajibu muhimu  
katika hii kazi.*

*Mmissionari wa kale Samuel Smith  
akishiriki Kitabu cha Mormoni*



utakaofuata. Kunyweni vidonge vyenu vya vitamini. Pumzikeni. Itakuwa ya kufurahisha.”<sup>3</sup>

Kwa kukubaliana na tangazo la Rais Nelson kwamba Urejesho unaendelea, tumeona mabadiliko mengi muhimu katika Kanisa kuanzia wakati alipokuwa Rais wake. Miongoni mwa hayo ni kupangwa upya kwa akidi za ukuhani, kuhudumu kuchukua nafasi ya ufundishaji wa nyumbani na wa kutembelea, na kuanzishwa kwa kujifunza injili kunakolenga nyumbani, na kusaidiwa na Kanisa.<sup>4</sup> Mabadiliko zaidi yamefanyika tangu wakati huo, na zaidi yanakuja.

### **Mfano kutoka Afrika Magharibi**

Ushuhuda wangu wa asili ya Urejesho unaendelea uliathiriwa na miaka mitano ambayo nilihudumu katika Urais wa Eneo la Afrika Magharibi. Kuanzia wakati nilipokuwa mvulana, nimekuwa na ushuhuda wa injili. Lakini

cha Mormoni na nyenzo zingine za Kanisa katika mikutano yao ya kanisani. Walisali kwa ajili ya siku ambayo Kanisa lingienda Ghana. Alijiunga na vijana wengine ambao walizunguka nchini Ghana na kufundisha injili jinsi ilivyopatikana katika nyenzo zetu. Mara tu wamisionari walipowasili mwaka 1978, alibatizwa siku ya kwanza wakati ubatizo wa Watakatifu wa Siku za Mwisho ulipofanyika Ghana.

Mapema katika wakati wa Fred kama muumini, alihudhuria mazishi ya jamaa ambaye alikuwa chifu wa kikabila. Hapo aligundua kwamba mpango wa familia ulikuwa kumtawaza awe chifu mpya. Akifahamu kuwa wadhifa kama huo ungemsababisha yeye kufanya vitu ambavyo havikubaliani na imani yake ya injili, alikimbia baada ya maziko na kukataa wadhifa ambao ungemletea umaarufu na mali.

Wakati Hekalu la Accra lilipowekwa wakfu, wote wawili James na Fred walisafiri zaidi ya

wakati nilipoishi Afrika, nilishirikiana na baadhi ya Waafrika wa Magharibi wa kwanza kukubali injili. Pia niliona Kanisa likienea kwa haraka kote barani, pamoja na mamia ya kata na vikingi vikiundwa, mahekalu na majumba ya mikutano yakifurika kwa waumini waaminifu, na wanawake na wanaume wema wakiikumbatia, kwa mioyo yao yote, injili ya urejesho. Mbele ya macho yangu niliona kutimizwa kwa unabii wa Joseph Smith kwamba Kanisa “litajaza ulimwengu.”<sup>5</sup>

Waumini wawili waaminifu kama hao, James Ewudzie na Frederick Antwi, walinisaidia siku moja Accra Ghana katika Hekalu. Miaka michache kabla ya wamisionari Watakatifu wa Siku za Mwisho kuwasili Ghana, James alikuwa sehemu ya kikundi cha watu 1,000 ambao walitumia Kitabu

masaa manne, kwenda tu, kila wiki ili waweze kuwa wahudumu wa hekaluni. Nilipotekeleza ibada pamoja nao, nilijawa na hisia za historia ambazo zilinizunguka. Nikitambua historia ya Kanisa katika Afrika ambayo wawili hao waliwakilisha, nilihisi ilifanana na kuwa na John Taylor au Wilford Woodruff au waumini wengine wa Kanisa wa mwanzo wakiwa pamoja nami tukizifanya ibada hizo.

Nilichoshuhudia, kupata uzoefu, na kuhisi katika Afrika Magharibi ilikuwa ni sehemu ya kile Bwana alichomwambia Henoko kitafanyika: “Na haki nitaishusha kutoka mbinguni; na ukweli nitaueneza kutoka duniani, ili kutoa ushuhuda wa Mwanangu wa Pekee; . . . na haki na ukweli nitavifanya viifagie dunia kama vile kwa gharika, ili kuwakusanya wateule wangu kutoka pande nne za dunia.” (Musa 7:62).

*Fred Antwi, muumini mwanzilishi wa  
Kanisa kule Ghana*



Niliona haki na ukweli vikifagia kote katika bara la Afrika na wateule wakikusanywa kutoka upande huo wa ulimwengu. Ushuhuda wangu wa Urejesho uliongezeka kwa sababu nilishuhudia sehemu hiyo muhimu ya Urejesho ikifanyika mbele ya macho yangu.

Pia niliona kitu kingine kuhusu Urejesho unaoendelea: imani changamfu na nguvu za kiroho miongoni mwa waumini Waafrika. Nimemsikia Mzee David A. Bednar wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili akisema, “Kirtland [Ambapo Watakatifu wa Siku za Mwisho walishi katika miaka ya 1830] haipo tu Ohio. Pia ipo katika Afrika.” Watu wengi wanajiunga na Kanisa katika Afrika kutokana na uzoefu wao binafsi wenye nguvu wa kiroho. Hao waumini wapya huleta nguvu ya kiroho na uhitaji wa kujifunza injili zaidi. Kwao Urejesho unaendelea katika hali ya binafsi. Wanapojifunza zaidi na zaidi kuhusu Kanisa, kweli za injili zinazidi

Mama, amefundisha, “Kufanya maagano ni ishara ya moyo wenye kukubali; kushika maagano, ishara ya moyo wa uaminifu.”<sup>6</sup>

Kwa kufanya na kushika maagano, hatuji-tayarishi tu kwa ajili ya uzima wa milele, lakini pia tunasaidia kutayarisha na kuimarisha kile ambacho Bwana anakiita “watu wangu wa agano” (Mafundisho na Maagano 42:36). Tunafanya

*Vijana wakipanga foleni kuingia katika Hekalu la Accra Ghana*



kujitokeza kwenye mtazamo wao. Hilo pia ni kweli kwetu sisi wote tunapozidi kupanua uelewa wetu wa injili.

### **Njia Tatu za Kusaidia katika Urejesho Unaoendelea**

Mungu ametupatia nafasi nzuri kabisa ya kutekeleza wajibu muhimu katika hii kazi. Bwana alisema kwamba “mwili [wa Kanisa] unahitaji kila kiungo” (Mafundisho na Maagano 84:110). Waumini wote wa Kanisa wana baraka ya kushiriki katika Urejesho huu unaoendelea. Tunaweza kufanya hivyo?

**Njia moja ya kushiriki ni kufanya na kushika maagano matakatifu.** Ibada, ikijumuisha ibada za hekaluni, hazina maana mpaka watu hasa wanapofanya na kuyashika maagano yanayohusika na ibada hizo. Dada Bonnie Parkin, aliyekuwa Rais Mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Akina

maagano na Mungu na kuwa sehemu ya watu Wake wa agano kupitia ubatizo, uthibitisho, sakramenti, ukuhani wa Melkizedeki, na ibada za hekaluni.

**Njia ya pili ambayo tunaweza kushiriki katika Urejesho unaoendelea ni kwa kutimiza wito na majukumu tunayopokea.** Hivyo ndivyo Kanisa linavyosonga mbele. Walimu waliojitolea hufundisha injili kwa watoto, vijana, na watu wazima. Akina dada na akina kaka wahudumiaji huwajali waumini binafsi wa Kanisa. Urais na uaskofu hutoa mwongozo kwa vigingi, wilaya, kata, matawi, akidi, mashirika, madarasa, na vikundi. Viongozi wa vijana wanawajali wasichana na wavulana. Makarani na makatibu huhifadhi taarifa muhimu ambayo inarekodiwa mbinguni, na wengine wengi hutekeleza majukumu muhimu katika kuwatarisha watu kwa ajili ya uzima wa milele na Ujio wa Pili wa Mwokozi.

*Kama ilivyofundishwa na Rais Nelson, tunayo nafasi na jukumu la kusaidia katika kukusanyika ambako kunafanyika pande zote za pazia.*

**Njia ya tatu ambayo tunaweza kushiriki katika Urejesho ni kusaidia kukusanya Israeli.** Kutoka siku za mapema za Urejesho, hii imekuwa sehemu muhimu ya kazi hii. Kama ilivyofundishwa na Rais Nelson, tunayo nafasi na jukumu la kusaidia katika kukusanyika ambako kunafanyika pande zote za pazia. Katika ujumbe wake wa kuhitimisha katika mkutano wake mkuu wa kwanza kama Rais wa Kanisa, Rais Nelson kwa maneno mafupi dhahiri alisema, “Ujumbe wetu kwa ulimwengu ni rahisi na wa kweli: tunawaalika watoto wa Mungu wote kutoka pande zote mbili za pazia waje kwa Mwokozi wao, wapokee baraka za hekalu takatifu, wawe na furaha ya kudumu, na kustahili uzima wa milele.”<sup>7</sup>

Kukusanya Israeli kutoka upande huu wa pazia inamaanisha kazi ya umisionari. Kila mmoja wetu ambaye anaweza kutumikia misheni anapaswa kufikiria juu ya nafasi hiyo

Kabla ya kuondoka, alikubali kwamba tungeweza kuzungumza kwa dakika chache. Tulienda katika darasa ambapo tulipendekeza tusali pamoja. Baada ya kupiga magoti, tulimomba asali. Baada ya sala alisimama akitokwa na machozi na kusema, “Ni sawa, nitabatizwa.” Na dakika chache baadaye alibatizwa. Mwaka uliofuata alifunga ndoa na Sebastiano Caruso, na waliwalea watoto wanne, wote ambao

*Mzee na Dada Curtis pamoja na baadhi ya wanafamilia wa familia ya Caruso*



kwa umakini. Ninaichukulia kama baraka kubwa kwamba niliweza kutumikia misheni Italia wakati ambapo Kanisa lilikuwa changa mno huko. Matawi yetu yalikutana katika kumbi za kupanga, na tulitumaini ya kwamba siku moja vingingi na kata vingepatikana huko. Nilishuhudia waanzilishi jasiri wakija Kanisani na kuunda msingi wa kukusanya Israeli katika nchi hiyo kuu.

Mmoja wao alikuwa Agnese Galdiolo. Sisi wote tulihisi Roho kwa nguvu wakati alipofundishwa masomo ya umisionari. Lakini, hata kuhisi Roho huyo, alijua kwamba familia yake wangepinga vikali kubatizwa kwake. Wakati fulani, hata hivyo, akiwa amejawa na Roho, alikubali kubatizwa. Lakini akabadili uamuzi wake asubuhi ya ubatizo wake uliokuwa umeratibiwa. Alikuwa mapema kwenye ukumbi wa kupanga ambapo angebatizwa kutuelezea kwamba kwa sababu ya upinzani kutoa kwa familia, hangeweza kubatizwa.

walitumikia misheni na wanaendelea tangu wakati huo kuhudumu Kanisani.

Agnese na Sebastiano pia walitumikia misheni, Sebastiano kama rais wa misheni. Wakati nilipotumikia misheni ya pili Italia, miaka 25 baada ya ile ya kwanza, niliweza kuona kile ambacho familia ya Caruso na waanzilishi wengine walikuwa wamefanya ili kupanua ufalme wa Mungu huko. Mimi na wamisionari wangu tulifanya kazi kujenga Kanisa, tukiwa na ndoto kuwa siku moja hekalu lingejengwa Italia. Fikiria furaha yangu kwamba sasa tuna Hekalu la Roma Italia.

Kuna furaha chache ambazo zinaweza kulinganishwa na furaha ya umisionari. Ni baraka kuu iliyoje kuzaliwa wakati ambapo tunaweza kushiriki kwa furaha katika Urejesho unaoendelea kwa kusaidia kukusanya Israeli!

Furaha ya umisionari, bila shaka, haipatikani tu kwa wamisionari pekee. Kila mmoja wetu

*Ubatizo wa Agnese Galdiolo*





Eliza R. Snow, kiongozi wa awali wa Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama



anaweza kusaidia katika uongofu na kuwarejesha katika uhudhuriaji kamili dada zetu na kaka zetu kwa kufanya kazi pamoja na wamisionari. Tunayo nafasi ya kukusanya Israeli kupitia kuwaalika wengine waje na waone na kwa kushirikiana na wale wanaofundishwa.

**Ni kupitia kazi ya hekaluni na historia ya familia ambapo tunasaidia kukusanya Israeli upande mwingine wa pazia.** Kwa miaka mingi imekuwa jukumu letu takatifu kuifanya kazi hii. Kabla ya kifo cha Joseph Smith, Watakatifu walifanya ubatizo kwa niaba ya wafu, na wachache walipokea endaumenti zao na kuunganishwa. Baada ya kukamilika kwa Hekalu la Nauvoo, endaumenti kwa ajili ya wanaoishi zilianza kwa bidii. Endaumenti na kuunganishwa kwa ajili ya mababu pia zilianza katika mahekalu ya Utah.

Eliza R. Snow, mshiriki mkuu katika mchakato huo wa urejesho, alielewa umuhimu wa sehemu hiyo ya Urejesho. Alitumia muda

mwingi katika nyumba ya endaumenti, akisaidia katika ibada huko.<sup>8</sup> Wakati wa utembeleaji mmoja wa Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama mnamo mwaka 1869, aliwafundisha dada zake, “Nimekuwa nikitafakari juu ya kazi kuu tunayohitajika kuifanya, hata kusaidia katika wokovu wa wanaoishi na wafu. Tunataka kuwa . . . wenza wastahiki wa Mungu na Walio Watakatifu.”<sup>9</sup>

Na, bila shaka, kupatikana kwa ibada za hekaluni kumepanuliwa pakubwa sana na ujenzi wa mahekalu mengi kote ulimwenguni, na mengi yanakuja.

Pamoja na vifaa ambavyo tunavyo kwa matumizi yetu, kazi ya hekalu na historia ya familia inaweza kuwa sehemu ya kawaida ya kushiriki kwetu katika Urejesho unaoendelea. Nimevutiwa na kushiriki katika kazi ya historia ya familia kwa miaka mingi, lakini vifaa vya mtandaoni vimeimarisha pakubwa mafanikio yangu katika

kutuma majina hekaluni. Nina kumbukumbu takatifu za kuketi kando ya meza nyumbani kwetu kule Ghana na kutafuta majina ya mababu zangu wa kutoka Uropa ambayo mimi na mke wangu tungeweza kupeleka katika Hekalu la Ghana Accra. Nafasi hiyo ya furaha imetufuata katika sehemu zingine ambazo tumetumwa.

Kupitia kwa Nabii Joseph Smith, Mungu alianza mchakatio wa “kukamilisha urejesho wa mambo yote yaliyonenwa kwa vinywa vya manabii watakatifu tangu mwanzo wa ulimwengu” (Mafundisho na Maagano 27:6). Urejesho huo umeendelea hadi leo pale Mungu “ambapo sasa anayafunua” na “atayafunua mambo mengi makuu na muhimu yahasuyo Ufalme wa Mungu” (Makala ya Imani 1:9). Ninashukuru sana kwamba tuna nafasi ya kushiriki katika Urejesho huu unaoendelea. ■

*“Kama unadhani Kanisa lime-  
rejeshwa kikamilifu, unashu-  
hudia mwanzo tu. Kuna mengi  
zaidi yanakuja.”*  
—Rais Nelson

#### MUHTASARI

1. Ona Waefeso 1:10; Mafundisho na Maagano 27:13.
2. Ona Danieli 2:35–45; Mafundisho na Maagano 65.
3. Russell M. Nelson, katika “Latter-day Saint Prophet, Wife and Apostle Share Insights of Global Ministry,” Okt. 30, 2018, newsroom.ChurchofJesusChrist.org.
4. Ona “Mwelekeo wenye Uvuvio,” *Liahona*, Mei 2019, 121.
5. *Mafundisho ya Marais wa Kanisa: Joseph Smith* (2007), 137.
6. Bonnie D. Parkin, “Kwa Utakatifu wa Moyo,” *Liahona*, Nov. 2002, 103.
7. Russell M. Nelson, “Acha Tusonge Mbele,” *Liahona*, Mei 2018, 118–19. Kwa kurudia wazo hilo, Rais Nelson alisema katika mkutano mkuu mwaka mmoja baadaye: “Na acha tuweke wakfu na kuweka wakfu upya maisha yetu ili kumtumikia Mungu na watoto Wake—pande zote za pazia” (“Maneno ya Kutamatisha,” *Liahona*, Mei 2019, 112).
8. Nyumba ya endaumenti ilijengwa katika Temple Square wakati Hekalu la Salt Lake lilipokuwa likijengwa. Ilipowekwa wakfu mwaka 1855, nyumba ya endaumenti ilitumika kwa ajili ya ibada za hekaluni hadi kufikia 1889.
9. Eliza R. Snow, address to Lehi Ward Relief Society, Okt. 27, 1869, Relief Society Minute Book, 1868–79, Church History Library, 26–27.

*Ni kupitia kazi ya hekaluni na historia ya familia ambapo tunasaidia kukusanya Israeli upande mwingine wa pazia.*

# WALIKUWA NA TUMAINI LA KUJA KWA KRISTO—NA PIA SISI TUNAWEZA KUWA NALO

Manabii katika Kitabu cha Mormoni walikuwa na tumaini kwamba Kristo angekuja. Kwa kusoma maneno yao, tunaweza kuwa na tumaini sawa na hilo kwa ajili ya wakati Atakapokuja tena.

## Na Mindy Selu

Magazeti ya Kanisa

**N**i maneno gani yanakujia akilini wakati unapofikiria kuhusu Kitabu cha Mormoni?

Wanefi, Walamani, -ites wa aina nyingine?

Vita, nyika, ole?

Toba, ukombozi, haki?

Yesu Kristo?

Tumaini?

Pasaka ni wakati mzuri zaidi wa kufikiria upya ujumbe wa Kitabu cha Mormoni. Muhimu zaidi, ujumbe kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwokozi na Mkombozi wetu. Kwa sababu Yake, tunaweza hatimaye kuwa huru kutoka kwenye uchungu wa mwili na nafsi. Kutoka kifo na dhambi. Tunaweza kushinda kila kitu kibaya ulimwengu unachotutupia.

Kwa urahisi, tunaweza kuwa na tumaini.

Tumaini—tumaini la kweli, linalolenga kwa Yesu Kristo—liliwatia msukumo manabii wa kale kuweka kumbukumbu kwenye bamba za dhahabu ambazo zingekuwa Kitabu cha Mormoni. Yakobo anatuambia “Kwani, kwa madhumuni haya tumeandika vitu hivi, ili wajue kwamba tulijua kuhusu Kristo, na *tulikuwa na matumaini ya utukufu* wake miaka mia mingi kabla ya kuja Kwake” (Yakobo 4:4; msisitizo umeongezwa).

Yakobo alitaka tujue kwamba yeye—na manabii wengine ambao waliweka kumbukumbu—walijua kuhusu kuja kwa

Kristo. Mamia ya miaka kabla ya kuja Kwake! Na waliongozwa kuwa na tumaini hilo kutoka kwenye maneno ya manabii *wao* waliyosoma. Yakobo anaeleza, “na sio tu sisi pekee tuliokuwa na tumaini la utukufu Wake, lakini pia manabii wote watakatifu ambao walikuwa mbele yetu.

“Tazama, walimwamimi Kristo na kumwabudu Baba katika jina Lake, na pia sisi tunamwabudu Baba katika jina Lake. . . .

“Kwa hivyo, tunawachunguza manabii, na tunao ufunuo mwingi na roho ya unabii; pamoja na mashahidi hawa wote tunapokea tumaini, na imani yetu haiwezi kuti-ngishwa” (Yakobo 4:4–6; ona pia 1 Nefi 19:21; Yakobo 7:11; Mosia 3:13; Helamani 8:16).

Tumaini ambalo walipata kutoka kwa yote mawili uzoefu wao wenyewe na unabii waliosoma katika maandiko uliwatayarisha kwa ajili ya siku ambayo Kristo angekuja. Vilevile, manabii leo hii wanatuhimiza tujitayarisha kwa ajili ya wakati Kristo atakaporudi tena. Ikiwa tunapaswa kuwa na tumaini sawa na hilo, sisi pia tunahitaji “kuwachunguza manabii, na [kutafuta] kuwa na ufunuo mwingi na roho ya unabii.” Ushuhuda wao wa Yesu Kristo hauta-imarisha tu wetu lakini pia utatusaidia kujitayarisha kwa ajili ya ujio Wake.



## Lehi

“Kwa hivyo, ni muhimu sana kuwajulisha wakazi wa dunia kuhusu vitu hivi, ili wajue hakuna binadamu anayeweza kuishi karibu na Mungu, bila fadhili, na rehema, na neema za Masiya Mtakatifu, ambaye anatoa maisha yake mwilini, na kuichukua tena kwa uwezo wa Roho, ili alete ufufuo wa wafu, akiwa wa kwanza kufufuka.”

**2 Nefi 2:8**

## Nefi

“Na tunazungumza kuhusu Kristo, tunafurahia katika Kristo, tunahubiri kuhusu Kristo, tunatoa unabii kuhusu Kristo, na tunaandika kulingana na unabii wetu, ili watoto wetu wajue asili ya kutegemea msamaha wa dhambi zao.”

**2 Nefi 25:26**



## Alma

“Na atakwenda, na kuteseka maumivu na masumbuko na majaribio ya kila aina; na hii kwamba neno litimizwe ambalo linasema atabeba maumivu na magonjwa ya watu wake.

“Na atajichukulia kifo, ili afungue kamba za kifo ambazo zinafungu watu wake; na atajichukulia unyonge wao, ili moyo wake ujae rehema, kulingana na mwili, ili ajue kulingana na mwili jinsi ya kuwasaidia watu wake kulingana na unyonge wao.”

**Alma 7:11-12**

## Amuleki

“Na hivyo dhabihu kubwa na ya mwisho itakuwa Mwana wa Mungu, ndio, isiyo ya mwisho na milele.

“Na hivyo ataleta wokovu kwa wote ambao wataamini katika jina lake; hii ikiwa kusudi la hii dhabihu ya mwisho, kufungua tumbo la rehema, ambayo hupindua haki, na kuwafungulia wanadamu njia ya kupata imani na toba.

“Na hivyo rehema yaweza kutosheleza matakwa ya sheria, na kuwazungushia mikono ya usalama, wakati yeye ambaye hatumii imani hata kuweza kutubu ana-wekwa mbele ya sheria yote yenye kudai haki, kwa hiyo, yeye tu aliye na imani hata kuweza kutubu analetwa kwenye mpango ule mkuu na wa milele wa ukombozi.”

**Alma 34:14-16**

## Samweli Mlamani

“Kwani tazama, lazima kwa kweli afe kwamba wokovu uje; ndio, inampasa yeye kwa lazima kwamba afe, ili kutimiza ufufuo wa wafu, kwamba kwa hiyo sababu binadamu waletwe kwenye uwepo wa Bwana.

“Ndio, tazama, hiki kifo huleta kutimiza ufufuo, na hukombo binadamu wote kutokana na kifo cha kwanza—hicho kifo cha roho; kwani binadamu wote, kwa sababu ya kuanguka kwa Adamu wakito-lewa kutoka uwepo wa Bwana, wanafiki-riwa kama waliokufa, kwa vitu vya kimwili na vitu vya kiroho.

“Lakini tazama, ufufuko wa Kristo unakombo binadamu, ndio, hata binadamu wote, na huwarejesha kwenye uwepo wa Bwana.”

**Helamani 14:15-17**

## Mfalme Benyamini.

"Na ataitwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. . . .

"Na lo, anawajia walio wake, ili wokovu uwafikie watoto wa watu hata kupitia imani kwa jina lake; . . .

"Na atafufuka siku ya tatu kutoka kwa wafu. . . .

"Kwani tazama, na pia damu yake inalipiza dhambi za wale ambao wameanguka kwa sababu ya dhambi ya Adamu, ambao wameaga dunia bila kuelewa nia ya Mungu juu yao, au ambao wametenda dhambi bila kujua."

**Mosia 3:8-11**



## Mormoni

"Nataka mjue kwamba lazima muelimike kuhusu babu zenu, na mtubu dhambi zenu zote na mao-vu, na kuamini katika Yesu Kristo, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, na kwamba aliuawa na Wayahudi, na kwa uwezo wa Baba amefufuka tena, kwa kufanya hivyo amepata ushindi juu ya mauti; na pia kupitia kwake uchungu wa kifo umetolewa.

"Na anatumiza ufufuo wa wafu, ambako binadamu lazima atainuliwa kusimama mbele ya kiti cha hukumu.

"Na ameleta kutimizwa ukombozi wa ulimwengu, ambako yule ambaye atapatikana bila makosa mbele yake katika siku ya hukumu atakubaliwa kuishi kwenye uwepo wa Mungu katika ufalme wake, kuimba sifa zisizo na mwisho na jamii ya waimbaji wa juu, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, ambao ni Mungu mmoja, katika hali ya furaha ambayo haina mwisho."

**Mormoni 7:5-7** ■

# Pasaka Ina Maana Gani Kwangu Mimi?

**S**iku ya Pasaka tunashe-rehekea “siku muhimu sana katika historia”<sup>1</sup>—Ufufuo wa Mwokozi wetu Yesu Kristo. Tukio hili ni kitovu cha mpango wa furaha wa Baba wa Mbinguni.

Katika maisha ya kabla ya dunia, Yesu Kristo alichaguliwa kuwa Mwokozi wetu. Aliahidi kutoa njia ya sisi kusamechewa dhambi zetu na kurudi nyumbani kwetu mbinguni.

Asubuhi hiyo ya Pasaka ya kwanza, Yesu alitimiza ahadi Yake. Alishinda kifo. Kama matokeo, “Yeye ni nuru na uzima wa ulimwengu; ndio, nuru isiyu na mwisho, ambayo haiwezi kutiwa giza; ndio, na pia uzima usio na mwisho, kwamba hakutakuwa tena na kifo” (Mosia 16:9).

Ni baraka gani ambazo Ufufuo unaleta kwako?

## MUHTASARI

1. Dieter F. Uchtdorf, “Tazama Mtu!” *Liahona*, Mei. 2018, 108.
2. Russell M. Nelson, “Tunaposonga Mbele Pamoja,” *Liahona*, Apr. 2018, 7.

## Toba

Yesu Kristo anamuuliza kila mmoja wetu, “Je mtarudi kwangu sasa, na kutubu dhambi zenu, na kugeuka ili niwapo-nye?” Anaahidi, “Yeyote atakayekuja, nitampokea” (3 Nefi 9:13–14). Unahisi vipi unapotubu?





### Ufufuo

Kifo hakiepekiki, lakini ushindi wa Mwokozi dhidi ya kifo unahakikisha kwamba sote tutafufuliwa—mwili na roho vikiunganishwa tena katika mwili mkamilifu (ona Alma 11:43). Ni jinsi gani ufahamu wa Ufufuo unakupa tumaini?



### Uzima wa Milele

Upatanisho wa Mwokozi unasababisha uzima wa milele, au kuinuliwa kuwezekane. Ili kupokea baraka hii, ni lazima tutii amri. Rais Russell M. Nelson ameita njia inayoelekea kwenye uzima wa milele “njia ya agano.”<sup>2</sup> Ni sharti tufanye nini ili kufuata njia hii inayoelekea kwenye uzima wa milele?

THE GOOD SHEPHERD, GREY DAY GOLGOTHA, NA EVERY KNEE SHALL BOW, NA J. KIRK RICHARDS  
EMPTY GARDEN TOMB, NA STEVE HART

# Kwa Nini Mfalme Benyamini Anatumia Tuwe Kama Mtoto Mdogo?

APRILI 13-19

## Mosia 1-3


Je, umewahi kujisikia j moyo wako ukilainika wakati ambapo umemta-zama mtoto? Watoto kwa kawaida hunena kutoka moyoni na huonesha upendo na kauli rahisi za imani. Mwokozi alifundi-sha, “Yeyote ajinyenyeke-shaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni” (Mathayo 18:4).

Hii inaweza kuwa sababu moja ya Mfalme Benyamini kuwataka watu wake kumvua mwanadamu wa kawaida na kuwa kama vile watoto (ona Mosia 3:19).

Ni kwa jinsi gani tunaweza kuwa kama watoto? Rejelea Mosia 3:19 ili kujaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia maneno ambayo mfalme Benyamini alitumia kuelezea mtu ambaye ni kama mtoto.

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_
6. \_\_\_\_\_

*Kuwa kama mtoto mdogo kunatuwezesha kumkaribia Kristo na kupata uzoefu wa furaha ya kuwa Watakatifu kupitia Upatanisho Wake.*



### MJADALA

Tafuta sifa kama za Kristo kutoka kwa mashujaa unaowapenda zaidi kutoka kwenye Kitabu cha Mormoni. Unawezaje kufuata mfano wao?



**K**atika Kitabu cha Mormoni, watu wana- itwa kwa majina mengi— Waneffi, Walamani, na Waanti-Nefi-Lehi ni baadhi tu. Lakini Mfalme Benyami- ni alitaka watu wake waitwe kwa jina la juu, takatifu zaidi—jina la Yesu Kristo.

Hivi ndivyo tunavyoweza kudumisha jina la Mwokozi likiwa “limeandikwa daima mioyoni [mwetu]” (Mosia 5:12):

**MJADALA**

Unafanya nini kila siku kuha- kikisha ya kwamba unahifadhi jina la Kristo likiwa limeandi- kwa katika moyo wako?

# Inamaanisha Nini Kuwa na Jina la Kristo Kuandikwa Katika Mioyo Yetu?



**FANYA MAAGANO KUPITIA UBATIZO**

Wakati wa ubatizo, tunaagana na Mungu kujichukulia juu yetu jina la Kristo. Unafikiri hiyo ina maana gani? (Ona Mosia 18:8–9.)



**SHIRIKI SAKRAMENTI**

Tumeamriwa kushiriki sakramenti kwa ustahiki kila wiki. Wakati wa sakramenti, tunafanya upya agano letu la kujichukulia juu yetu jina la Yesu Kristo (ona Moroni 4:3).

**TENDA KAMA MFUASI WA KRISTO**

Maagano yetu yanatutaka kutii amri. Vitendo vyetu vinapaswa kuonesha nia yetu ya kumfuata Yesu Kris- to na kuwa kama Yeye. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kuendelea kuitwa kwa jina Lake. Hivi ndivyo tunavyo- weza kudumisha jina la Kristo likiwa limeandikwa daima mioyoni mwetu (ona Mosia 5:12).



## Baraka Pekee Ndiyo Niliweza Kutoa

**N**ilimaliza chuo cha mafunzo ya sheria karibu na wakati ambapo binti yangu alikuwa akisherehekea mwaka wa kwanza wa kuzaliwa. Mimi na mke wangu tulikuwa tuna-subiri kusherehekea kuhitimu kwangu, siku ya kuzaliwa ya binti yetu, na nafasi mpya ambazo tungepata, lakini hakuna kilichofanyika kulingana na mipango yetu.

Nilijikuta bila kazi muda mfupi baada ya kumaliza shahada yangu na nilikuwa na wakati mgumu kupata kazi. Mara, changamoto za kiuchumi zikaja. Kuwa na sherehe ndogo ya siku ya kuzaliwa ingekuwa vigumu.

Baada ya mazungumzo mengi na mke wangu, tulikubali hali yetu. Haikuwa rahisi kwangu kama baba kutokuwa na uwezo wa kununua hata zawadi ndogo kwa ajili ya binti yangu na kuona mke wangu mpendwa akihisi kukata tamaa.

Sikuelewa kilichokuwa kikifanyika.

Nilisali na kumwomba Baba wa Mbinguni anisaidie kuelewa kile ambacho Alitarajia nifanye. Ghafla, kana kwamba sauti ilinena akilini mwangu, nilisikia maneno yafuatayo: “Unamiliki kitu chenye thamani kuliko mali yote iliyopo humu duniani. Unamiliki ukuhani. Ni baraka ipi bora unaweza kumpa binti yako kuliko baraka ya ukuhani?”

Machozi yalijaa machoni mwangu

*Kana kwamba sauti ilinena akilini mwangu, nilisikia: “Unamiliki kitu chenye thamani kuliko mali yote iliyopo humu duniani.”*

nilipofikiria kuhusu maana ya ukuhani kwangu mimi. Moyo wangu ulijawa na shukrani wakati nilipofikiria kwamba ukuhani ni nguvu ambayo inaweza kuileta pamoja familia yangu milele.

Nilishiriki hisia zangu pamoja na mke wangu. Nilimwambia kwamba kumpatia baraka ya ukuhani binti yangu ilikuwa kitu pekee ambacho ningeweza kutoa. Sote tuliamua kwamba hilo lingelela furaha na amani kwake, na hilo lingetoshwa.

Siku ya kuzaliwa kwa binti yetu, marafiki, jamaa, na majirani walileta keki na mapambo ya kawaida. Tulikuwa

na shukrani kusherehekea siku hii maalum pamoja na wale tunaowapenda. Usiku huo, niliweka mikono yangu juu ya kichwa cha binti yangu na kumpa baraka. Nili-mbariki kwa kila kitu Roho wa Bwana alichoniongoza kusema.

Bado tunapitia kipindi cha mabadiliko na changamoto kuhusu kosa kazi na fedha. Lakini hata katikati ya huzuni na kukata tamaa, amani na faraja huja kwetu kupitia Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Sina wasiwasi kwamba kuwa muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho na kufikia nguvu za ukuhani ni baraka. Ilikuwa kitu pekee ambacho ningeweza kumpa binti yangu katika siku yake ya kuzaliwa, na hiyo ilitosha. ■

**Jonathan Mafra Sena de Santana,  
Santa Catarina, Brazil**



# Ndege Mdogo Alinikumbusha

**N**ilikuwa na miaka 26 wakati mimi na mume wangu tulipompoteza mtoto wetu wa kwanza. Kennedy aligunduliwa kuwa na uvimbe wa ubongo wakati alipokuwa na umri wa miezi 13 tu. Baada ya upasuaji mara tatu, mifululizo mitano ya tibakemikali, na madawa mengi na matibabu, aliaga dunia mikononi mwetu akiwa na umri wa miezi 20.

Nilivunjika moyo kumpoteza msichana wangu mdogo, mrembo, mwenye ari ya kujua, na mwenye nguvu. Ni kwa jinsi gani hili lilitokea? Ningewezaje kusonga mbele? Nilikuwa na maswali kadhaa, lakini sikuwa na majibu yoyote. Siku chache baada ya mazishi, mimi na mume wangu tulite-mbelea eneo la kaburi, lilikuwa bado limefunikwa na maua na utepe wa rangi ya waridi kutoka kwenye mazishi.

Nilipokuwa nikifikiria juu ya binti yangu, nilimwona ndege mdogo sana, mchanga asiyeweza kupaa, akirukaruka juu ya nyasi. Ndege huyu alinikumbusha kuhusu Kennedy kwa sababu alipenda wanyama. Ndege huyo alirukaruka juu ya kaburi na kucheza kwenye utepe na maua. Nilitabasamu, nikifahamu hivi ndivyo Kennedy angetaka. Ndege huyo kisha alirukaruka na kunikaribia. Siku-thubutu kusonga. Ndege huyo mdogo alirukaruka karibu nami, akaulalia mguu wangu, akafumba macho, na kulala.

Ni vigumu kwangu kueleza hisia nilizokuwa nazo kwa wakati huo. Nilihisi kana kwamba nilikuwa

nikikumbatiwa na Kennedy. Nisingeweza kumkumbatia binti yangu, lakini ndege huyu mdogo—kiumbe cha Baba wa Mbinguni—kingeweza kupumzisha kichwa chake juu yangu,

sawa katika maisha, . . . na wakati inao-nekana kwamba labda tuko peke yetu kabisa, kwa kweli tunabarikiwa na neema nyororo ya Bwana” (“Neema Nyororo za Bwana,” *Liahona*, Mei 2005, 100).



*Nilipokuwa nikifikiria juu ya binti yangu, ndege mdogo sana, mchanga asiyeweza kupaa, alirukaruka juu ya nyasi akinikaribia.*

kunikumbusha kwamba Baba wa Mbinguni alielewa uchungu wangu na siku zote angekuwepo kuja kunifariji na kunisaidia katika majaribu haya.

Mzee David A. Bednar wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alisema, “Wakati ambapo maneno hayawezi kutupa faraja tunayohitaji . . . , wakati mantiki na akili haviwezi kuleta uelewa wa kuto-sha kuhusu udhalimu na kutokuwa

Bado sikupata majibu ya maswali yangu yote, lakini neema hii nyororo ilinihakikishia kwamba mimi na Kennedy wote tunapendwa na Baba wa Mbinguni na kwamba kupitia dhahibu ya upatanisho ya Mwana Wake, Yesu Kristo, nina tumaini kwamba Kennedy, mume wangu, na mimi siku moja tutakuwa pamoja tena kama familia. ■

**Laura Linton, Utah, Marekani**

## Yenye Thamani Kuliko Bangili ya Fedha



*Asubuhi moja, niligundua kwamba bangili yangu ya fedha ilikuwa imepotea. Moyo wangu ulikuwa na huzuni kwa sababu bangili hii ilikuwa ya thamani kwangu.*

**W**akati nilipoombwa kuongoza mjadala katika Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama kuhusu mwaliko wa Mwokozi kulisha kondoo Wake, niliamua kwamba kama nilitaka kuwatia moyo akina dada, ni sharti nifanye jambo kwa ajili ya mmoja wa kondoo Wake.

Nilitafuta ujasiri na kumwalika dada asiyeshiriki kikamilifu kuhudhuria shughuli ya Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama pamoja nami. Alikubali mwaliko wangu na tulikuwa na wakati mzuri. Nilihisi kuwa huu ulikuwa mfano mwema, na nilikuwa na hamu ya kushirikiki uzoefu wangu. Lakini Bwana alikuwa na mengi ya kunifundisha.

Asubuhi moja nilipokuwa nikijiandaa, niligundua kwamba bangili yangu ya fedha ilikuwa imepotea. Nili kuwa nimepewa bangili hii kama zawadi kwenye siku ya kuzaliwa nilipokuwa

nazuru Ufaransa, kwa hivyo ilikuwa na maana maalum kwangu. Nilianza kuitafuta mahali ambapo palikuwa na uwezekano mkubwa kupatikana, lakini sikuipata. Kisha nilijiambia kwamba kama ningesali tu, ningeweza kuipata bangili yangu kwa haraka.

Baada ya kusali, nilitafuta kila mahali. Kwa muda wa siku mbili nilisali kwa dhati na kutafuta kwa bidii. Nilimlilia Baba wa Mbinguni anisaidie kuipata, lakini sikuipata. Moyo wangu ulikuwa na huzuni kwa sababu bangili hii ilikuwa ya thamani kwangu.

Jioni moja mwanangu alisali pamoja nami kando ya kitanda changu. Baada ya sala yetu, aliokota kitu fulani na kunipa. Ilikuwa bangili yangu! Alikuwa ameipata chini ya kitanda. Kwa namna fulani sikuiona nilipoitafuta. Nilililia kwa furaha kuipata tena.

Ghafla, wazo lilinijia: “Je, wewe unasali kwa dhati namna hii kwa niaba ya dada zako wa Kanisani? Je, wao ni wa thamani kwako kama bangili yako? Vipi kuhusu dada zako nje ya Kanisa? Unasali kwa niaba yao pia?”

Wakati niliposhiriki uzoefu wangu wa bangili yangu iliyokuwa imepotea katika Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama, tulikuwa na mjadala mzuri. Niliwaambia akina dada kwamba wakati Mwokozi anapotuomba tuwalishe kondoo Wake, ni lazima tukumbuke kwamba “thamani ya nafsi ni kubwa mbele za Mungu” (Mafundisho na Maagano 18:10). Anatumata tuwajali wale walio karibu na sisi na kupenda, kujali, na kusali kwa nguvu zetu zote kwa ajili yao. Wakati tunapofanya hivyo, tutagundua kwamba kila mtu ana thamani kubwa zaidi kuliko bangili ya fedha. ■

**Sylvie Houmeau, Quebec, Kanada**

# "Tazama Kile Imani Ndogo Inachoweza Kufanya?"

*Tulikimbia kulielekea gari huku dhoruba ikisonga kwa kasi upande wetu.  
"Acha tusali," mwana wetu mdogo alisema.*

**K**itambo kidogo, mimi na mke wangu tulisafiri na wana wetu wawili wadogo kwenda Ufaransa kute-mbelea maeneo ambayo nilikuwa nime-tumikia kama mmisionari. Tulitembelea matawi ya Kanisa ambapo nilikuwa nimetumikia na kufurahia na waumini ambao niliwafundisha. Pia tulitembelea maeneo ya kihistoria.

Eneo moja lilikuwa mahame ya Château de Châluca. Kasri hili la kale lilishambuliwa na kuharibiwa pakubwa karne nyingi zilizopita. Mimea ilikuwa imemea kuzunguka mahame hayo, na njia ya kufika pale ilikuwa imesonga na yenye mwinuko mkali. Tulikuwa na wakati mgumu kukwea, lakini ilitosheleza juhudi zetu mara tulipowasili.

Wavulana walifurahia kushuka kati-ka kile kilichokuwa kwa wakati mmoja gereza la chini ya ardhi na juu kabisa kwenye kile kilichokuwa kimesalia kwenye kuta za kasri. Kasri hilo lilichangamsha fikra zao jinsi tu lilivyokuwa limefanya kwangu miaka 24 kabla.

Wakati tulipokuwa huko, dhoruba ya majira ya jua ilitokea kwa mbali. Ilikaribia kwa kasi. Mawingu meusi na radi vilitanda angani, na kufuatiwa na milio mikubwa ya ngurumo.

Tulikimbia kulielekea gari huku dhoruba ikisonga kwa kasi upande wetu. Punde, mbubujiko, mkali wa mvua ulitulowesha na njia ikageuka kuwa tope. Tulikuwa na wasiwasi kwamba

tungepoteza mwelekeo na kuanguka chini ya mteremko mkali, wa mawe.

Tuliona kimbilio fulani kwenye miti pembeni mwa njia. Tulijibana pamoja chini ya kimbilio na kuwaza ingechukua muda kiasi gani kusubiri kushuka chini.

"Acha tusali," mwana wetu mdogo alisema.

Alijitolea kusali na akasali kwamba mvua ingetulia ili tuweze kushuka chini ya mlima kwa usalama. Alitutazama na kusema, "Sasa kile tunachohitaji sana ni imani ya kutosha."

Nilieleza kwamba sala huwa hazifanyi kazi siku zote kwa namna hiyo.

"La," alisema, "itatulia kwa takriban ndani ya dakika 10!"

Baada ya takriban dakika 10, mvua ilitulia.

"SAWA, twendeni!" alisema.

"Kama tutaondoka sasa hivi, mvua itaanza tena na tutazuiliwa," mwana wetu mkubwa alisema.

"Hapana!" mdogo alijibu. "Twendeni!"


Tulipita katika sehemu za njia zilizokuwa zimekauka, tukishikilia vichaka na matawi tulipokuwa tukisonga. Karibu na gari, tulisali kutoa shukrani. Punde, mvua ilianza tena.

"Unaona kile imani ndogo inachoweza kufanya?" mwana wetu alisema kwa unyenyekevu.

Alitufundisha somo kuu siku hiyo. ■  
**Godfrey J. Ellis, Washington, Marekani**







Na Mzee  
Kyle S. McKay  
Wa Sabini

# Badiliko Kuu la Moyo

**K**ufuatia Anguko la Adamu, magonjwa na dhambi viliingizwa duniani. Vyote viwili vinaweza kusababisha mauti katika falme zao husika. Kati ya magonjwa yote, labda hakuna ulioenea au unaodhuru kama saratani. Katika baadhi ya mataifa, zaidi ya theluthi moja ya idadi ya watu watapata aina fulani ya saratani, na inachangia karibu robo ya vifo vyote.<sup>1</sup> Saratani kawaida huanza na seli moja, ndogo sana inaweza tu kuonekana kwa kutumia hadubini. Lakini ina uwezo wa kukua na kuenea haraka sana.

Wagonjwa wa saratani hufanyiwa matibabu ili kupunguza makali ya saratani. Kupungua kikamilifu kuna maana kwamba hakuna ushahidi wowote wa ugonjwa huo ambao unaonekana. Hata hivyo, wataalamu ni wepesi kusema kwamba ingawaje mgonjwa anaweza kuwa anaonekana kupata nafuu, haimaanishi kwamba amepona.<sup>2</sup> Hivyo basi, ingawa kupata nafuu kunaleta faraja na matumaini, wagonjwa wa saratani daima hutumainia kitu ambacho ni zaidi ya kupata nafuu—wanatumaini kupona. Kulingana na chanzo kimoja, “Kuthibitisha mtu amepona kutokana na saratani, mtu anapaswa kusubiri kuona ikiwa saratani itarudi, kwa hivyo, wakati ndicho kipengele muhimu. Kama mgonjwa atabakia katika kupata nafuu kwa miaka kadhaa, saratani inaweza kuwa imepona. Aina fulani ya saratani zinaweza kutokea tena baada ya miaka mingi ya kupata nafuu.”<sup>3</sup>

Dhambi inaharibu, inalemaza, na kuangamiza nafsi. Dhambi ni chanzo kikuu—kwa kweli, chanzo cha pekee—cha kifo cha kiroho.

Matibabu ya dhambi ni toba.

## Ugonjwa na Dhambi

Kama jinsi saratani ilivyo na madhara makubwa kwenye mwili, dhambi ina madhara zaidi kwa nafsi. Dhambi kawaida huanza kidogo kidogo—wakati mwingine udogo usioweza kutambulika—lakini ina uwezo wa kukua kwa haraka. Inaharibu, kisha kulemaza, na kisha kuangamiza nafsi. Ni chanzo kikuu—kwa kweli, chanzo cha pekee—cha kifo cha kiroho katika uumbaji wote. Matibabu ya dhambi ni toba. Toba ya kweli inafaa kwa asilimia 100 katika kumpatia mtenda dhambi nafuu, au kusababisha msamaha wa dhambi. Msamaha huu huleta faraja na furaha kwa nafsi. Hata hivyo, kupokea

msamaha wa dhambi na kuwa huru kutokana na dalili na athari zake haimanishi kwamba mtenda dhambi ameponywa kikamilifu. Kuna kitu fulani kuhusu moyo wa mwanadamu aliyeanguka ambacho kinawezesha au kinafanya iwe rahisi kutenda dhambi. Hivyo basi, dhambi inaweza kutokea tena, hata baada ya miaka mingi ya kupata nafuu. Kusalia ukiwa na nafuu, au kwa namna nyingine, kudumisha msamaha wa dhambi, ni muhimu kwa ajili ya kupona kikamilifu.

### **Kusafishwa na Kuponywa**

Analojia hii inatusaidia kuelewa kwamba kiroho, hatuasafishwi tu kutokana na dhambi lakini pia tunaponywa kutokana na utendaji wa dhambi. Vita ambavyo vinapiganisha nia yetu ya kutenda mema dhidi ya asili yetu ya kutenda maovu inaweza kuchosha. Tukiwa waaminifu, tutakuwa washindi si tu kwa sababu tumeilazimisha nia yetu juu ya asili yetu, lakini kwa sababu tumesalimisha nia yetu kwa Mungu na Amebadili asili yetu.

Mfalme Benyamini alifundisha “Kwani mwanadamu wa kawaida ni adui kwa Mungu, na amekuwa tangu kuanguka kwa Adamu, na atakuwa, milele na milele, asipokubali ushawishi wa Roho Mtakatifu, na kumvua mtu wa kawaida . . . kupitia upatanisho wa Kristo aliye Bwana” (Mosia 3:19). Katika kujibu haya na mafunzo mengine, watu wa Benyamini walisali, “Ewe tuhurumie, na utumie damu ya upatanisho wa Kristo kwamba tupokee msamaha wa dhambi zetu, *na* mioyo yetu isafishwe” (Mosia 4:2; msisitizo umeongezwa). Baada ya wao kusali, Bwana alijibu ombi lao lililokuwa na sehemu mbili. Kwanza, “Roho wa Bwana aliwashukia, na wakajazwa na shangwe, wakiwa wamepokea msamaha wa dhambi zao, na kupata amani katika dhamira zao” (Mosia 4:3).

Alipoona kwamba watu wake walikuwa “wamepokea msamaha,” Mfalme Benyamini aliwahimiza kupata tiba kamili kwa kuwafundisha jinsi ya kuhifadhi msamaha (ona Mosia 4:11–30). “Kama mtafanya haya,” aliahidi, “mtapokea furaha daima, na kujazwa na upendo wa Mungu, na daima kuhifadhi msamaha wa dhambi zenu” (Mosia 4:12).

Watu waliamini na kujifunga wenyewe kwa maneno ya Mfalme Benyamini, ambapo Bwana alijibu sehemu ya pili ya sala yao—kwamba “mioyo [yao] isafishwe.” Kwa shukrani na kusifu, watu walilia kwa sauti, “Roho wa Bwana Mwenyezi . . . ameleta mabadiliko makuu ndani yetu, au mioyoni mwetu, kwamba hatuna tamaa ya kutenda maovu tena, lakini kutenda mema daima” (Mosia 5:2). Mfalme Benyamini alieleza kwamba badiliko hili kuu lilimaanisha kwamba walikuwa wamezaliwa na Mungu (ona Mosia 5:7).

### **“Je, Inafanywa Vipi?”**

Nabii Alma alifundisha kwamba ni sharti tutubu *na* tuzaliwe tena—tuzaliwe na Mungu, tubadilike katika mioyo yetu (ona Alma 5:49).

Tunapoendelea kutubu, Bwana ataondoa dhambi zetu zote *na* Ataondoa kile ambacho kiasili kinasababisha au kuleta dhambi ndani yetu. Lakini, kwa maneno ya Enoshi, “Bwana, je, inafanywa vipi?” (Enoshi 1:7). Jibu ni rahisi, tena la kina na la milele. Kwa wale ambao wameponywa kutokana na hali yoyote, ya kimwili au kiroho, Bwana alisema, “Imani yako imekufanya mkamilifu” (ona Marko 5:34; Enoshi 1:8).

Badiliko kuu la moyo alilokuwa nalo Alma lilifanyika “kulingana na imani yake,” na mioyo ya wafuasi wake ilibadilika wakati “walipoweka tumaini lao katika Mungu wa kweli na anayeshi” (Alma 5:12, 13). Mioyo ya watu wa Mfalme Benyamini “ilibadilishwa kwa imani katika jina [la Mwokozi]” (Mosia 5:7).

Kama tutakuwa na imani kama hii, ili tuweze kumwamini Bwana kwa moyo wetu wote, ni sharti tufanye kile kinacholeta imani na kisha tufanye kile ambacho imani inaleta. Miongoni mwa vitu vingi ambavyo huleta imani, katika muktadha wa badiliko hili la moyo, Bwana

*Mabadiliko haya makuu  
katika mioyo yetu yana-  
fanyika ndani yetu;  
hayafanywi na sisi.*

amesisitiza mfungo, sala, na neno la Mungu. Na ingawaje imani huleta vitu vingi, toba ni tunda lake la kwanza.

Fikiria mistari miwili ifuatayo kutoka kitabu cha Helamani ambayo inaonesha kanuni hizi. Kwanza, tunasoma kuhusu watu ambao “walifunga na kuomba kila wakati, na wakapokea nguvu . . . wakawa imara zaidi na imara katika





***Kwa sababu ya Upatanisho wa Yesu Kristo, hatusafishwi tu kutokana na dhambi; tunaweza pia kuponywa kutokana na utendaji dhambi.***

imani yao ya Kristo . . . hata kwenye kusafishwa na utakaso wa mioyo yao, utakaso ambao huja kwa sababu ya wao kumtolea Mungu mioyo yao” (Helamani 3:35). Kisha, kutoka kwa Samueli Mlamani, tunajifunza, “Maandiko matakatiifu, ndio, utabiri wa manabiii watakatiifu, . . . unawangoza . . . kuwa na imani kwa Bwana, na kwenye toba, imani na toba ambavyo, huwaletea mabadiliko katika mioyo” (Helamani 15:7).

**Kumtegemea Mungu**

Hapa ni sharti tupumzike na kukiri kwamba badiliko hili kuu tunalolizungumzia linafanyika *ndani* yetu; halifanywi *na* sisi. Tuna uwezo wa kutubu, kubadili mienendo yetu, tabia zetu, hata tamaa na imani yetu, lakini hatuna nguvu na uwezo wa kubadili asili yetu. Kwa ajili ya badiliko hili kuu, tunamtegemea kikamilifu Mwenyezi Mungu. Ni Yeye ambaye kwa neema anasafisha mioyo yetu na kubadili asili yetu “baada ya kutenda yote tunayoweza” (2Nefi 25:23). Mwaliko Wake ni imara na wa kweli: “Tubuni, na mje kwangu na moyo wa lengo moja, na *nitawaponya* [ninyi]” (3 Nefi 18:32; msisitizo umeongezwa).

Athari ya kuponywa kutoka kuwa mwenye dhambi ni kwamba “tubadilishwe kutoka hali [yetu] ya kimwili na kuanguka, hadi hali ya utakatifu . . . kuwa wana na mabinti zake; Na hivyo [sisi] tunakuwa viumbe vipya”

(Mosia 27:25, 26). Nyuso zetu zinanururisha Nuru ya Kristo. Aidha, maandiko yanatambua kwamba “kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi” (1 Yohana 5:18). Hii si kwa sababu hatuwezi kutenda dhambi, lakini kwa sababu sasa ni asili yetu *kutotenda* dhambi. Hayo ni mabadiliko makuu, kwa kweli.

Inapaswa kukumbukwa kwamba kupata mabadiliko makuu ya moyo ni mchakato ambao hufanyika baada ya muda, sio wakati mmoja. Kawaida mabadiliko hufanyika polepole, wakati mwingine yanayoongezeka bila kutambulika, lakini ni ya kweli, ni yenye nguvu mno, na yanahitajika.

Kama hujapata uzoefu wa mabadiliko makuu kama hayo, ningekuuliza: Je, umetubu na kupokea msamaha wa dhambi zako? Je, wewe husoma maandiko matakatiifu? Je, wewe hufunga na kusali mara kwa mara, kwamba uweze kuwa imara zaidi na zaidi katika imani ya Kristo? Una imani ya kutosha kumwamini Bwana kwa moyo wako wote? Unasimama imara katika hiyo imani? Je, wewe unachunga mawazo, maneno, na vitendo vyako na kushika amri za Mungu? Kama mtafanya vitu hivi, daima mtafurahia na kujazwa na upendo wa Mungu na daima kuhifadhi msamaha wa dhambi zenu. Na ukiendelea kuwa na nafuu, utaponywa, kupata tiba, na *kubadilishwa!*

Yesu Kristo ana uwezo wa kutusafisha kutokana na dhambi zetu na pia kutuponya kutokana na utendaji dhambi. Ana uwezo wa kuokoa, na kwa sababu hiyo, Ana uwezo wa kubadili. Kama tutampa mioyo yetu, kuwa na imani kwa kufanya mabadiliko yote ambayo tuna uwezo wa kuyafanya, Atatumia uwezo Wake ndani yetu kufanya mabadiliko haya makuu ya moyo (ona Alma 5:14). ■

**MUHTASARI**

1. Ona Stacy Simon, “Facts & Figures 2019: US Cancer Death Rate Has Dropped 27% in 25 Years,” American Cancer Society, Jan. 8, 2019, cancer.org.
2. Ona “Remission: What Does It Mean?” webMD.com.
3. Cathy Sweat, *The Gates to Recovery* (2019).

# Kuboresha Uzoefu Wetu wa Hekaluni

## Na Urais wa Kwanza

“Taji ya kito ya Urejesho ni hekalu takatifu. Ibada zake na maagano matakatifu ni ya msingi katika kuwaandaa watu walio tayari kumkaribisha Mwokozi katika Ujio Wake wa Pili.”<sup>1</sup>

Kwa wakati ufaao, Urais wa Kwanza umefanya marekebisho kwenye ibada za hekaluni na taratibu ili kuboresha uzoefu wa hekaluni kwa waumini na kuwasaidia wote wanaoingia kuhisi uhusiano wa karibu na Mungu katika mazingira haya matakatifu.

Kama sehemu ya uzoefu wa hekaluni, washiriki huvalia mavazi maalum yenye umuhimu wa kimafundisho na kiishara ambayo asili yake inapatikana katika ibada ya hekaluni katika Agano la Kale (ona Mambo ya Walawi 8 na Kutoka 28).

Marekebisho kadhaa yamefanywa kwa mavazi maalum ya ibada ya hekaluni. Marekebisho haya hayaashirii mabadiliko kwenye ishara za hekaluni au mafundisho lakini yamekusudiwa kufanya ibada ya hekaluni kuwa rahisi zaidi, ya kuliwaza, na ya kupatikana kwa urahisi kwa kuyafanya mavazi kuwa rahisi kuvaliwa, kuyatunza, na bei nafuu.

Baadhi ya marekebisho haya ni pamoja na:

- Mtindo rahisi zaidi wa shela na joho.
- Kuondoa plastiki iliyotiwa ndani ya kofia na tai kutoka kwenye kofia na shela.
- Kutumia kitambaa cha kudumu zaidi ambacho kinatumika kwenye joho, kofia, na mshipi, ambacho kinavisadia kudu mu kwa muda mrefu zaidi na kuvifanya rahisi kuvitunza.

Tunatumaini marekebisho haya yatasaidia kuboresha uzoefu huu mtakatifu kwa ajili yako unapofanya ibada ya hekaluni kuwa sehemu ya kawaida katika maisha yako. ■

### MUHTASARI

1. Russell M. Nelson, “Maneno ya Kutamatisha,” *Liahona*, Nov. 2019, 120.

“Marekebisho yoyote ambayo yamefanywa kwenye ibada na taratibu hayabadili asili takatifu ya maagano ambayo yanafanyika [ndani ya hekalu]. Marekebisho yanawezesha maagano kupandwa ndani ya mioyo ya watu wanaoishi katika nyakati na hali tofauti.”

Rais Russell M. Nelson, mkutano wa mafunzo ya viongozi katika mkutano mkuu, Okt. 2019.



## MAJIBU KWA MASWALI YA KAWAIDA

### **Je, ninaweza kuendelea kutumia mavazi maalum ya ibada ambayo niko nayo?**

Ndiyo. Mitindo ya awali inaweza kuendelea kutumika mpaka pale itakapohitajika kubadilishwa.

### **Ni njia zipi bora za kutupa mavazi maalum ya ibada ambayo ni kuukuu?**

“Kutupa mavazi maalum kuukuu ya hekaluni, waumini wanapaswa kuyaharibu kwa kuyakatakata vipande vidogo vidogo ili matumizi ya asili yasiweze kutambuliwa” (*Handbook 2: Administering the Church* [2010], 21.1.42).

### **Je, naweza kurekebisha mavazi ya sasa kulingana na marekebisho mapya?**

Ndiyo. Maelezo ya ziada kuhusu jinsi gani yanapatikana kwenye [store.ChurchofJesusChrist.org/ceremonialclothing](https://store.ChurchofJesusChrist.org/ceremonialclothing) wakati unapoingia ukitumia

akaunti yako ya uumini au kwa kutembelea [Distribution Services](https://DistributionServices.org) na kumuuliza karani wa duka.

### **Naweza kutoa msaada mavazi maalum ya ibada ambayo ni kuukuu?**

Wakati inapofaa, unaweza kutoa kwa ukarimu mavazi yaliyotumika kwa wanafamilia au marafiki ambao wamepokea endaumenti. Hata hivyo, mavazi maalum, bila ya kujali hali yake, hayapaswi kutolewa msaada kwa hekalu, Deseret Industries, au sehemu yoyote ya kubadilishana mavazi.

### **Nawezaje kupata mavazi mapya?**

Kwa ajili ya maelezo kuhusu bei na upatikanaji katika eneo lako, nenda kwenye [store.ChurchofJesusChrist.org/ceremonialclothing](https://store.ChurchofJesusChrist.org/ceremonialclothing) au tembelea [Distribution Services](https://DistributionServices.org).

# Vijana Wakubwa

## Katika Sehemu Hii

44 Jinsi Vijana Wakubwa Wanavyoleta Tofauti katika Urejesho Unaoendelea.

## Kidijitali Pekee

Unafikiri Huna Lengo kama Kijana Mkubwa? Fikiria Tena

Na Cesar Gervacio

Kutumia Jina Kamili la Kanisa Ilikuwa Vigumu lakini Ilistahili

Na Lauri Ahola

Kupata Furaha katika Kufanya Kazi ya Bwana

Kujenga Ufalme katika New Caledonia

Na Mindy Selu

## Tafuta makala hizi na nyingine zaidi:

- Kwenye [liahona.ChurchofJesusChrist.org](http://liahona.ChurchofJesusChrist.org)
- Katika [VW kila wiki](http://VW.kila.wiki) (kwenye sehemu ya Vijana Wakubwa katika Gospel Library)

## Shiriki Hadithi Yako

Je, una hadithi ya kupendeza ya kushiriki? Au je, unataka kuona makala kuhusu mada fulani? Kama ndivyo, tunataka kusikia kutoka kwako! Unaweza kuwasilisha makala yako au jibu lako kwenye [liahona.ChurchofJesusChrist.org](http://liahona.ChurchofJesusChrist.org).

## Tunaweza Kueneza Nuru ya Injili

**U**jana mkubwa ni wakati wa kukua, fursa nyingi, na nafasi ya kuanza kujenga maisha yako. Na hilo linaweza kuwa la kuchosha mno, kulisimua, na kuogofya yote kwa wakati mmoja (hakika imekuwa hivyo kwetu sisi).

Lakini hata kama hatuna majibu ya maswali yote muhimu ya maisha, kuna kitu kimoja ambacho tuna uhakika nacho—kwamba **vijana wakubwa siku zote wamekuwa nguvu muhimu katika Urejesho unaoendelea wa Kanisa la Yesu Kristo.**

Katika kupanga sehemu ya mwezi huu, tulizungumza na vijana wengi wakubwa kuhusu kushiriki kwao katika ukusanyaji wa Israeli. Na tumenyenyekezwa sana na upendo wao wa dhati na kujitolea kwao kwa ajili ya injili ya Yesu Kristo. Bila kujali hali zao, hawa **vijana Watakatifu wanaelewa wajibu mkuu walio nao katika kipindi hiki cha mwisho.** Katika “Jinsi Vijana Wakubwa Wanavyoleta tofauti katika Urejesho Unaoendelea” katika ukurasa wa 44, unaweza kusoma jinsi vijana wakubwa kutoka India, Hungary, Barbados, Australia, na Marekani wanavyoutayarisha ulimwengu kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Mwokozi.

Katika makala ya kidijitali pekee, Cesar anatoa umaizi kuhusu jinsi **tunavyoweza kupata lengo letu na kuwa viongozi.** Lauri anazungumza kuhusu baraka tunazopata kwa kutii ushauri wa nabii. Vijana wengine wakubwa wanashiriki uzoefu wao wa huduma ya hekaluni, kuhudumu, historia ya familia, na kazi ya umisionari. Na tunashiriki mfano kutoka kwa kijana mkubwa kutoka New Caledonia unaoonesha jinsi **waumini wa umri mdogo wanavyofanya kazi ya Bwana katika maeneo madogo ya Kanisa.**

Popote ulipo na bila kujali hali yako ilivyo, **unaweza kuchangia pakubwa katika kukusanya Israeli zaidi ya vile unavyodhania.** Kama vijana wakubwa, sisi ni viongozi wa baadaye wa Kanisa hili. Na cheche ya juhudi zetu leo itawaka na kueneza nuru ya injili kote ulimwenguni kesho.

Kwa moyo wa dhati,

Chakell Wardleigh na Mindy Selu

Wahariri wa Magazeti ya Kanisa sehemu ya vijana wakubwa



PICHA NA WESTON C. COLTON

# Jinsi Vijana Wakubwa Wanavyoleta Tofauti katika **Urejesho Unaoendelea**

---

Vijana wakubwa siku zote wamekuwa na wajibu muhimu katika kazi ya wokovu.

---

**W**akati wowote unaposikia mwaliko kutoka kwa kiongozi wa Kanisa kushiriki katika Urejesho unaoendelea au kusaidia katika kukusanya Israeli, je umewahi kufikiria, “Ni nini naweza nika-fanya? Mimi ni mtu mmoja tu,” “Mimi nina umri mdogo sana,” “Mimi sina ndoa,” au “Mimi sijui vya kutosha. Ni tofauti gani ninaweza kuleta?”

Kila mmoja wetu ana mawazo kama hayo akilini mara kwa mara. Lakini jaribu kunyamazisha mashaka haya binafsi unaposoma sentensi chache zinazofuata:

- Joseph Smith alikuwa na umri wa miaka 22 tu wakati alipoanza kutafsiri Kitabu cha Mormoni.
- Oliver Cowdery alikuwa pia na miaka 22 na John Whitmer alikuwa na miaka 26 (na wote wawili walikuwa waseja!) wakati walipoanza kufanya kazi kama waandishi wa Joseph.
- Mwaka 1835, wakati Akidi ya kwanza ya Mitume Kumi na Wawili ilipoitwa, walitofautiana kwa umri kuanzia miaka 23 hadi 35.
- Wengi wa Watakatifu wa mwanzo ambao walijiunga na Kanisa na kueneza injili walikuwa vijana wakubwa.

Kwa jumla, Mungu alifanya kazi kupitia vijana wakubwa katika siku za mapema za Urejesho wa injili ya Yesu Kristo. Watu kama wewe.

Acha hilo lizame ndani yako.

Kanisa halingeweza kuenea kote duniani leo hii kama kila mtu angedhania kwamba hawezi kuleta tofauti. Na wewe—ndio, wewe!—ni sehemu ya kizazi kilichochaguliwa kuendelea kurejesha na kuongoza Kanisa la Yesu Kristo leo hii.



**JOSEPH SMITH,  
MIAKA 22**  
Alianza kutaf-  
siri Kitabu cha  
Mormoni

**OLIVER  
COWDERY,  
MIAKA 22**  
Alianza kufanya  
kazi kama mwa-  
ndishi wa Joseph.

**JOHN  
WHITMER,  
UMRI 26**  
Alianza kufanya kazi  
kama mwandishi  
wa Joseph.

## Ulitumwa Hapa. Sasa hivi. Kwa sababu fulani.

Wakati akizungumza kuhusu kizazi chetu, Rais Russell M. Nelson alifundisha, “mnaishi ndani ya ‘saa ya kumi na moja.’ Bwana ameta-ngaza kwamba huu ni wakati wa mwisho ambao Atawaita watumishi katika shamba Lake la mza-ibu kuwakusanya wateule kutoka pande zote nne za dunia. (Ona M&M 33:3–6.) Na wewe ulitumwa kushiriki katika ukusanyaji huu.”<sup>1</sup>

Fikiria kuhusu jeshi la wamisionari 65,000 wanaoshiriki injili siku nzima, kila siku, kote ulimwenguni. Fikiria kiuhusu vijana wakubwa wote ambao wanafanya maagano hekaluni, wakitumia ukuhani uliorejeshwa na baraka za hekaluni na wakiahidi kuwa waaminifu, kuimari-sha familia zao, na kuujenga ufalme wa Mungu duniani. Fikiria kuhusu vijana wakubwa wanao-hudumu kama viongozi wa Kanisa kote ulimwe-nguni. Fikiria kuhusu wale ambao wanasonga mbele kumfuata Yesu Kristo licha ya upinzani

---

Mungu alifanya kazi kupitia vijana wakubwa katika siku za mwanzo za Urejesho. Watu kama wewe tu.

---



Urejesho unahusu kutafuta ufunuo.

**VENNELA VAKAPALLI,**  
MIAKA 22, INDIA

wote dhidi yao. Vijana Wakubwa wamekuwa sehemu muhimu ya Urejesho toka mwanzo. Na Urejesho unaoendelea umekuwa sehemu muhimu ya maisha ya vijana wakubwa wengi ambao ni waumini wa Kanisa.

## Kile Urejesho Unachomaanisha Kwetu

Kwa wengi wetu, kushiriki kwetu kati-ka Urejesho kunatokana na kile ambacho urejesho umetufundisha sisi. Kwa Vennela Vakapalli, kijana mkubwa muongofu kutoka Andhra Pradesh, India, “Urejesho unahusu kutafuta ufunuo. Joseph Smith alitafuta ufunuo msituni. Alishauriana na Bwana, alisubiri apate jibu, alikuwa na subira. Hayo ndiyo ninayopenda.” Vennela anaeleza, “Kabla ya kusikia kuhusu Urejesho, Sikujua mengi kuhusu kutafuta ufunuo. Mojawapo ya vitu vikuu ambavyo hunishangaza mimi ni kiasi cha muda aliotumia kupata ufunuo kutoka kwa Mungu. Hicho ndicho nilichojifunza kuto-ka kwenye Urejesho.”

Ufahamu mwingi ambao huja na urejesho unafanya maisha yangu kuwa rahisi na tulivu.

**JACOB ROBERTS,**  
MIAKA 29, MAREKANI



Emma na Jacob Roberts, wenza wa umri mdogo kutoka Utah, Marekani, wanakubali kwamba Urejesho unahusu “ufunuo unaoendelea”—kwa ajili yetu na kwa ajili ya uli-mwengu—“kwamba tunaweza kuwa na nabii, msemaji hapa duniani kutoka kwa Mungu, kuhakikisha kwamba changamoto zozote uli-mwengu unazoleta, tuna mtu ambaye anafanya kazi na kusali na kuzungumza na Mungu kuhakikisha kwamba tuko tayari na tuna uwezo wa kukabiliana na changamoto zozote ulimwengu unazoleta wakati anapobadilika.”

“Ufahamu mwingi ambao huja na urejesho unafanya maisha yangu kuwa rahisi na tulivu,” anasema Jacob. Unakuja na hakikisho “kwamba kuna Mungu anayetupenda na kutulinda,” Emma anasema. “Nia Yake ni tuwe na furaha. Kama vijana wakubwa, tunaweza kumwamini Yeye kikamilifu na kumfuata kwa sababu tunajua lengo Lake ni sisi tuwe na furaha. Tunajua kwamba sisi ni viumbe wa milele, na hilo linanipa matumaini na imani nyingi, kwamba chochote ninachofanya hivi sasa na makosa yoyote ninayofanya hivi sasa, bado naweza kutubu na nina wakati huu wa kuendelea na kujifunza.”

Kutiwa moyo kwa aina hiyo pia kulimsaidia Ramona Morris, kijana mkubwa kutoka





Urejesho huleta amani kwa wale ambao wana maswali kuhusu maisha yao na mpango wa Mungu kwa ajili yao.

**RAMONA MORRIS,  
MIAKA 28, BARBADOS**

Barbados, wakati alipojifunza kuhusu Urejesho kwa mara ya kwanza. Miongoni mwa vitu vingine, alipata ushuhuda kwamba “Baba wa Mbinguni yuko pale kwa ajili yetu. Urejesho huleta amani kwa wale ambao wana maswali kuhusu maisha yao na mpango wa Mungu kwa ajili yao.”

Lakini hata kama kuelewa Urejesho kumeleta uwazi katika maisha yake, anakiri pia “kuwa mbali sana na makao makuu ya Kanisa, ni vigumu kuhusiana na injili, lakini kwa sababu nimekuwa na ushuhuda imara wa injili ya urejesho, ninajua kwamba mbali nilivyo, bado naweza kuhisi kuwa sehemu ya Urejesho, kwamba siko peke yangu.”

Na hayuko peke yake. Vijana wakubwa kote ulimwenguni wanashiriki katika Urejesho kupitia huduma ya hekaluni, historia ya familia, na kazi ya umisionari. Kwa uelewa wa ufunuo binafsi ambao tunapata kutokana na kujifunza kuhusu Ono la Kwanza la Joseph Smith na Urejesho, tunaweza

wote tukaendelea kutafuta kujua mapenzi ya Mungu na kile tunachoweza kufanya katika Urejesho unaoendelea.

## Vijana Wakubwa Wakiongoza Kanisa

Tunaweza kuwa vijana wakubwa, lakini tunaweza kuwa viongozi katika Kanisa sasa hivi. Licha ya kuwa muumini pekee wa Kanisa katika familia yake, Janka Toronyi kutoka Győr, Hungary, anaimarishwa na kushiriki kwa vijana wakubwa wenzake katika vipengele vingine vya Urejesho: “Marafiki zangu kadhaa wametumikia misheni, na imekuwa vizuri sana kuona maendeleo yao na kisha wanarudi na wanakua kabisa kupitia uzoefu wao. Ni uzoefu mzuri sana kwa ajili yetu sisi wote. Na siku zote ni ajabu kuwaona rafiki zangu vijana wakubwa waseja wakitumikia katika wito wao na wakati mwingine hata nafasi wanazotafuta wenyewe, kama kujitolea kuwa washauri katika mikutano ya FSY (Kwa

Urejesho unahusu kuwaimarisha waumini ambao tuko nao.

**JANKA TORONYI,  
MIAKA 24, HUNGARY**



---

Kwangu mimi, kushiriki katika Urejesho ni kuvisaidia vizazi vya siku za baadaye kuelewa jinsi injili inavyoweza kuwasaidia wao na wengine katika maisha yao.

**STEFANY JOSEPH,**  
**MIAKA 28, AUSTRALIA**

---



Ajili ya Nguvu kwa Vijana). Ninahisi kwamba Urejesho hauhusu tu kufundisha watu kuhusu injili—ni kuhusu kuwaimarisha waumini ambao tuko nao.”

Vijana wakubwa kule Hungary wanaelewa kwamba wao ni viongozi wa baadaye wa Kanisa. “Tunahitajika na tunahitaji kuwa tayari kutimiza jukumu, ambalo wakati mwingine linakuwa gumu,” Janka anakiri. “Bwana anaharakisha kazi na sisi ni sehemu yake. Wakati mwingine tunafikiria, ‘Nawezaje kufanya hili?’ Lakini ni vizuri kuona kwamba viongozi wetu wana imani kubwa na sisi. Inatia moyo kwa wale ambao wanapenda Kanisa na wana ushuhuda imara, kwa sababu tunajua kwamba siku moja tutawajibika. Ni lazima tuwajibikie maendeleo yetu ya kiroho sisi wenyewe.”

Sean na Stefany Joseph kutoka Magharibi mwa Australia wanashiriki katika Urejesho kwa kuwashauri vijana katika kata yao. “Kwangu mimi, kushiriki katika Urejesho ni kuvisaidia vizazi vya siku za baadaye kuelewa injili ni nini na jinsi inavyoweza kuwasaidia wao na

wengine kwenye maisha yao,” Stefany anasema. “Tunaweza tukasaidia kujenga msingi thabiti kwa ajili ya Kanisa katika nchi yetu baadaye.”

“Tunataka kuwasaidia vijana kupata ushuhuda wa Kitabu cha Mormoni na Joseph Smith na kutambua kwamba wao wenyewe hakika ni watoto wa Mungu,” Sean anaeleza. “Hatutaki kiwe tu ni kitu ambacho waliimba katika Msimingi—tunataka wajue hakika kwamba ni kweli.”

Kulingana na Vennela, kuishi injili India si rahisi kila wakati, lakini anajua uwezo wa vijana wakubwa waumini huko utawatia msukumo wengine na kusaidia Urejesho kusonga mbele. “Hapa, vijana wote wakubwa ni waaminifu. Wao hutafuta nafasi za kushiriki ushuhuda wao,” anasema. “Sisi ni kama watangulizi hapa India. Tunahama kutoka sehemu mbalimbali na hata baadhi yetu wanaziacha familia zao. Maisha yanaweza kuwa magumu hapa, lakini bado sisi huchagua kuishi injili. Maandiko yananipa tumaini, nguvu, na ujasiri mwingi.”

Haijalishi mahali tulipo, kama vijana waku-bwa, tunaweza kuendelea kuwa na ushawishi wenye nguvu juu ya Urejesho unaoendelea kupitia imani yetu na kujitolea kwenye injili.

## Siku za Baadaye za Kanisa: Ni Juu Yetu Sisi

Sisi ni siku za baadaye za Kanisa. Tuko katika vita vya mwisho. Baba wa Mbinguni anatute-gemea sisi kumsaidia kufanya kazi Yake—Kazi Yake ya kuleta mabadiliko ya milele. Anajua tuna uwezo wa kutosha kuendelea kusonga mbele na kupigana dhidi ya kila kitu ambacho adui ana nia ya kutumia. Na Shetani anapoteza tumaini. Anajua anapigana katika vita ambavyo atashi-ndwa kwa sababu kazi ya Bwana itashinda.

“Tunajua kwamba Bwana anaharakisha kazi na hakuna anayeweza kuisimamisha,” Janka anasema. “Tunajua itafanyika kwa vyovyote vile. Lakini lazima tuamue kama tutakuwa sehemu yake na kuisaidia kusonga mbele au kutazama kutokea pembeni. Tuna haki ya kujiamulia kuwa sehemu yake, na tuna ushuhuda wa kutu- zeshwa kuchagua haki na kuchagua kumfuata Kristo. Ni lazima tuwe sehemu yake.”

Kwa hivyo ni juu yetu kuchagua ni upande wa nani tuko.

Ni juu yetu kuwa na ujasiri wa kusimama kwa ajili ya kile tunachoamini.

Ni juu yetu kutafuta ufunuo binafsi kwa ajili ya maisha yetu.

Ni juu yetu kukubali changamoto ngumu tunazokabiliana nazo kuimarisha imani yetu katika Mwokozi.

Ni juu yetu kumfuata Yeye na kufanya kadri ya uwezo wetu kuwale- ta wengine Kwake.

Ni juu yetu kuvumilia hadi mwisho vizuri tuwezavyo.

Hakika tuko katika siku za mwisho. Na kuliongoza Kanisa katika kile Rais Nelson anachoita “kipindi chenye ushawishi mkubwa zaidi katika historia ya ulimwengu”<sup>2</sup> inaonekana kama jukumu gumu sana. Lakini fikiria kuhusu hilo—Baba wa Mbinguni alituamini vya kutosha na kutu- hifadhi sisi ili tuje duniani hasa kwa wakati huu, wakati huu ambapo tunakabiliana na majaribu yasiyohesabika na vivuta mawazo na dhana nyingi zinazopingana.

Kwa kututuma hapa katika kipindi hiki cha maana sana, Baba wa Mbinguni hakuwa anatupangia kufeli. Anajua uwezo wetu, nguvu zetu, ujasiri wetu, na hatimaye, Anajua tunaweza kuleta tofauti katika Urejesho wa Kanisa, bila kujali umri wetu na hali ya ndoa. Bila kujali majaribu yetu ni magumu kiasi gani, au jinsi isivyowezekana kuongoza na kushiriki injili kote ulimwenguni inavyoonekana, pamoja Naye kando yetu, ni nani ana- weza kupigana dhidi yetu? Atatuwezesha kutimiza yasiyowezakana. ■

### MUHTASARI

1. Russell M. Nelson, “Simameni kama Wanamilenia wa Kweli,” *Liahona*, Okt. 2016, 48.
2. Russell M. Nelson, “Simameni kama Wanamilenia wa Kweli,” *Liahona*, 46.

*Unaweza kupata hadithi zaidi za vijana wakubwa kutoka kote ulimwenguni wakishiriki katika Urejesho katika makala ya kidijitali pekee “Kupata Furaha katika Kufanya Kazi ya Bwana.”*





## Mimi ni mwongofu kwa Kanisa.

Mojawapo ya vitu ambavyo vilinivutia mwanzo ilikuwa shughuli za vijana. Hata sasa mimi bado nafurahia kutumia wakati pamoja na marafiki kutoka Kanisani ambao hushiriki burudani nzuri, ya aina ya kuinua. Mimi hufurahia hasa kutembelea Hekalu la Suva Fiji pamoja nao kila wiki.

Fiji kuna ushawishi mkubwa kutoka kwa makundi ya rika moja. Maduka huwa hayaulizi kitambulisho wakati wote ili kununua pombe, sigara, na vitu kama hivyo. Watoto huvinunua wakati wote. Inaweza kuwa vigumu kuchagua mema.

Mojawapo ya vitu ambavyo hunifanya kuwa imara ni ndugu zangu wadogo. Mimi ni mkubwa wao, kwa hivyo mimi huwafikiria kila wakati pale ninapojaribiwa kufanya jambo baya. Sitaki wafanye maamuzi mabaya kwa sababu ya kuona nikifanya kitu kibaya kwanza. Kabla mama yangu hajafariki, aliniomba niahidi kuwatunza ndugu zangu na siku zote kuwajali.

Kufikia sasa mimi ni muumini pekee wa Kanisa miongoni mwa ndugu zangu. Lakini mimi husali kwa niaba yao kila siku. Ninamshukuru Baba wa Mbinguni kwa kuwapa wao siku nyingine ya kuishi, na ninasali kwamba watapokea ufahamu wa injili Yake. Wananipa nguvu.

**Mikayla J.,** miaka 17, Fiji

### KATIKA SEHEMU HII



#### 52 **Imarisha Ushuhuda Wako Kupitia Ono la Kwanza**

Na Mzee Neil L. Andersen

#### 56 **Teksi, Mvulana wa shule, na jibu kwa Sala**

Na Sydney Chime Ihunwo

#### 58 **Kupata Imani Yangu Hatua Moja baada ya nyingine**

Na Mzee Edward Dube

#### 62 **Maswali na Majibu: Ono la Kwanza na Kitabu cha Mormoni**

#### 64 **Picha Nne kutoka Wiki ya Pasaka**



**Na Mzee Neil L. Andersen**

Wa Akidi ya Mitume  
Kumi na Wawili

---

# IMARISHA USHUHUDA WAKO KUPITIA ONO LA KWANZA

**WAKATI NILIPOKUWA NA UMRI WA MIAKA 16**, nilisafiri kutoka nyumbani kwetu Idaho kuhudhuria mkutano uliokuwa Pwani ya Mashariki ya Marekani, uliohudhuriwa na wavulana na wasichana kutoka majimbo yote 50 na mataifa takriban 40. Kabla ya hapo, ni mara chache nilikuwa katika hali ambapo imani na misimamo yangu vilinitofautisha.

Jioni moja katika mazingira yasiyo rasmi ya kikundi, mjadala ulitokea kuhusu baadhi ya imani na desturi za Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Kikundi kikubwa cha wanafunzi kilinigeukia na kuanza kuuliza maswali, baadhi ambayo yalikosoa imani yetu.

Hilo lilitokea ghafla. Lakini baada ya kutafakari kwa muda, nilianza kushiriki baadhi ya kanuni za msingi. Nilieleza

kwamba tuna Baba wa Mbinguni, kwamba sisi ni wana na mabinti Zake, na kwamba tuko duniani kukuza imani katika Yesu Kristo na kujithibitisha kwa kucha-gua wema dhidi ya uovu.

Kushiriki kanuni hizi kulinielekeza kwenye ushuhuda wa Joseph Smith. Wanafunzi wengine hawakuwa wameuliza kuhusu Joseph Smith, lakini nilijikuta nikielekea kwenye asili ya kwa nini niliamini kile nilichoamini. Nilipokuwa nikielezea juu ya kuonekana kwa Baba na Mwana katika Msitu Mtakatifu, ghafla kila mtu alinyamaza. Hisia takatifu ilipenya ndani ya chumba, na hisia kubwa ya nguvu za kiroho ilishuka juu yangu na juu ya maneno yangu.

Baadaye, wanafunzi kadhaa walinishukuru kwa ajili ya imani yangu thabiti. Baadhi hata walitaka maelezo zaidi kuhusu

Kanisa. Nilipokuwa nikirudi chumbani kwangu usiku huo, niligundua kwamba mtu ambaye tukio hili lilikuwa na ushawishi mkubwa juu yake alikuwa mimi. Nilikuwa nimehisi mimi mwenyewe nguvu za kutoa ushuhuda wa Mungu Baba, Yesu Kristo, na Ono la Kwanza.

Tangu tukio hilo zaidi ya miaka 50 iliyo-pita, nimeshuhudia nyakati nyingi kuhusu Baba, Mwana, na Nabii Joseph Smith. Katika matukio haya, nimehisi siku zote ushahidi wa kuthibitisha wa Roho Mtakatifu.

Ningependa kushiriki kanuni tatu ambazo nimejifunza kutoka kwenye uele-wa wangu wa kiroho wa Ono la Kwanza. Kanuni hizi zimeimarisha imani yangu kati-ka na tamaa yangu kumfuata Baba yetu wa Mbinguni na Mwana Wake Mpendwa. Ninatumaini zitawaimarisha pia.



*Ninaomba kwamba mtafuata mtindo wa Joseph wa kusali, mjifunze kweli alizojifunza, na muimarisha imani yenu katika Baba wa Mbinguni na Mwana Wake, Yesu Kristo.*



## KUTOKA ONO LA KWANZA, TUNAJIFUNZA KWAMBA VIUMBE HAWA WA SELESTIA WANATUFAHAMU KIBINAFSI, JINSI VILE WALIVYOMFAHAMU JOSEPH.

### 1. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu Ni Viumbe Tofauti

Kwa karne nyingi, wasomi wa kidini na wanafalsafa walikuwa wamefanya mdahalo wa asili ya Mungu Baba, Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu. Wengi waliamini ni Walikuwa kiumbe mmoja. Kwa sababu ya tukio la Joseph katika Msitu Mtakatifu miaka 200 iliyopita, tunajua ukweli halisi kuhusu asili ya Mungu.

Kwanza kabisa, Yu Hai! Pili, Baba na Mwana ni viumbe wawili tofauti,

watukufu, waliofufuka, wenye upekee. Baadaye, Joseph alifunza kwamba “Roho Mtakatifu hana mwili wa nyama na mifupa, bali ni mtu wa Kiroho. Kama isingekuwa hivyo, Roho Mtakatifu asingeweza kukaa ndani yetu” (Mafundisho na Maagano 130:22).

### 2. Sisi ni Wana na Mabinti za Mungu

Kupitia Ono la Kwanza na matukio mengine, nabii Joseph Smith alijifunza

kwamba Mungu si nguvu kutoka mbali ambaye aliumba ulimwengu na wakazi wake na kisha kuwasahau. Kiuhalisia, kila moja wetu ni “binti mpendwa [au mwana] wa wazazi wa mbinguni.”<sup>1</sup>

Tangazo juu ya familia linasema: “Wanadamu wote—wanaume na wana-wake—wameumbwa katika mfano wa Mungu. Kila mmoja ni mwana au binti mpendwa wa kiroho wa wazazi wa mbinguni, na, kama hivyo, kila mmoja ana asili takatifu na takdiri.”<sup>2</sup> Baba yetu ametangaza wazi takdiri hiyo: “Hii ni kazi yangu na utukufu wangu—kuleta kutokufa na uzima wa milele wa mwanadamu” (Musa 1:39).

Utambulisho wetu uko na Mungu, na tuko hapa duniani kuwa zaidi kama Yeye. Uelewa huu kutoka Ono la Kwanza uliniruhusu mimi kama mvulana kujua kwamba nilikuwa na Baba wa Mbinguni binafsi ambaye alinipenda na alinitaka nirudi Kwake.

### 3. Tunaweza Kusamehewa Dhambi Zetu

Mojawapo ya wasiwasi mkubwa wa Joseph ilikuwa msamaha wa dhambi zake. Katika simulizi moja ya Ono la Kwanza, Bwana alimwambia mtafutaji huyo mdogo wa ukweli: “Joseph, mwanangu, dhambi zako zimesamehewa. Enenda zako, enenda katika hukumu zangu, na ukazishike amri zangu. Tazama, mimi ni Bwana wa utukufu. Nilisulubiwa kwa ajili ya ulimwengu, ili wote watakaoliamini jina langu waweze kupata uzima wa milele.”<sup>3</sup>

Joseph alijifunza kwamba kupitia Upatanisho wa Yesu Kristo, angeweza kusamehewa dhambi zake na kuwa msafi



na bila doa mbele za Mungu. Alipewa ufahamu thabiti kwamba Yesu Kristo alijichukulia juu Yake dhambi na mizigo ya wale wote ambao waliwahi kuishi na watakaishi duniani.

Kutokana na Ono la Kwanza, tunajifunza kwamba kwa sababu ya neema ya Mwokozi, Yesu Kristo, sisi pia tunaweza kusamehewa dhambi zetu na siku moja kusimama tukiwa wasafi mbele za Baba.

#### 4. Baba Yetu wa Mbinguni Husikia na Kujibu Sala Zetu

Msituni siku ile katika mwaka 1820, Joseph alijifunza kwamba Baba wa Mbinguni husikia na kujibu sala. Baadaye, Joseph alisema, "Nilikuwa na imani kamili katika kupata mafunuo matakatifu, kama ambavyo awali nilikuwa nimepata" (Historia ya—Joseph Smith 1:29). Mfano wake unatufundisha kwamba tunaweza kumkaribia Baba yetu wa Mbinguni kupitia sala ili kupokea majibu yetu wenyewe.

Joseph alirudia mtindo huu wa sala tena na tena. Alikuwa na imani kwamba Baba wa Mbinguni angelisikia na kujibu sala zake. Alisali kuhusu vitu ambavyo inawezekana umesali juu yake.

Alisali kwa ajili ya hekima (ona Historia ya—Joseph Smith 1:12–13).

Alisali kwa ajili ya ubatizo (ona Historia ya—Joseph Smith 1:68).

Alisali kwa ajili ya uponyaji (ona Mafundisho na Maagano 121:1–4).

Alisali kwa ajili ya wamisionari (ona Mafundisho na Maagano 109:22).

Alisali kwa ajili ya Kanisa, waumini wake, na voingozi wake (ona Mafundisho na Maagano 109:71–76).

Na alisali kwa ajili ya familia yake (ona Mafundisho na Maagano 109:68–69).

Huu ni mtindo kwa ajili yetu Joseph aliotuonesha kwamba sote tunaweza kwenda kwa Baba yetu katika sala?

#### 5. Baba na Mwana Wanatufahamu Kibinafsi

Kutoka Ono la Kwanza, tunajifunza kwamba Viumbe hawa wa Selestia wanatufahamu kibinafsi, jinsi vile walivyomfahamu Joseph. Baba alimwita Joseph kwa jina na, "akimwonesha mwingine kwa kidole," akasema, "*Huyu ni Mwanangu Mpendwa. Msikilize Yeye!*" (Historia ya—Joseph Smith 1:17).

Baba na Mwana walifahamu mahitaji, wasiwasi, na matamano ya Joseph, jinsi vile Wanavyofahamu yetu. Pia wanajua mafanikio na huzuni yetu.

Katika ujana wangu, nilisali kwa ajili ya vitu vingi. Ninapotazama nyuma sasa, baadhi ya vitu hivyo si muhimu sana. Lakin vilikuwa muhimu kwangu wakati huo, na nilielewa tangu umri mdogo kwamba nilikuwa na Baba wa Mbinguni ambaye alinikiliza mimi. Sikupata siku zote jibu la haraka, lakini nilihisi kwamba katika wakati Wake na njia Yake Angejibu ombi langu katika njia iliyokuwa sawa kwa ajili yangu.

Kuwa na imani kwamba Mungu atazungumza nawe. Amini katika hizo hisia ambazo huja ndani kwa kina kwenye moyo wako. Nilikuja kuamini katika sala na kuelewa uwezo wake kwa sababu nilijua uzoefu wa Nabii Joseph Smith. Nilijua kwamba Mungu alijua jina langu na Angenijibu, jinsi vile anavyojua jina lako na atakujibu.

#### Ushuhuda

Kwa kiasi kikubwa katika miaka 68 ambayo nimeishi duniani, nimejaribu mtindo wa sala wa Joseph Smith. Kama wafuasi wote wa kweli wa Mwokozi, mimi pia nimepokea majibu kutoka mbinguni. Najua kuwa Yesu ndiye Kristo. Yeye ni Mwana wa Mungu. Alifufuka na yu hai leo. Ana uwezo wa kusamehe dhambi zetu. Kupitia imani, utiifu, na toba yetu, Anaweza kuturejesha salama nyumbani kwetu mbinguni.

Kama Mtume wa Bwana Yesu Kristo na shahidi Wake aliyetawazwa, ninashuhudia kwa uhakika na imani iliyothibitishwa na Roho Mtakatifu kwamba Baba na Mwana walimtokea Joseph katika Msitu Mtakatifu. Ninaomba kwamba mtafutata mtindo wa Joseph wa kusali, mjifunze kweli alizojifunza, na muimarisha imani yenu katika Baba wa Mbinguni na Mwana Wake, Yesu Kristo. ■

#### MUHTASARI

1. "Dhamira ya Wasichana," youngwomen.ChurchofJesusChrist.org.
2. "Familia: Tangazo kwa Ulimwengu," *Liahona*, Mei 2017, 145.
3. "Simulizi za Joseph Smith kuhusu Ono la Kwanza," josephsmithpapers.org.

# TEKSI, MVULANA WA SHULE, na JIBU LA SALA

*Tulikuwa na msukumo kwamba  
tungempata, kwa hivyo ni kwa  
nini hilo halikufanikiwa?*





RIELELEZO NA COREY EGBERT

## Na Sydney Chime Ihunwo

**S**iku moja mimi na mwenza wangu mmisionari tulipewa jina kwa ajili ya kumfundisha mwanaume ambaye aliishi katika kijiji kinachoitwa Tema, karibu na jiji zuri la Accra, Ghana. Nambari za nyumba katika kijiji hicho hazikuwa sahihi, kwa hivyo tulipewa maelezo yaliyokuwa yameandikwa kwenye karatasi kutusaidia kuipata nyumba hiyo.

Wakati tulipowasili katika kijiji, tulifuata maelezo yote lakini hatukuweza kumpata mwanaume huyo kwa sababu ilionekana kwamba kulikuwa na nyumba nyingi ambazo zililingana na maelezo hayo. Tukiwa tunahisi kukanganyikiwa, tuliambia kubisha milango katika ujirani ili kuuliza, lakini hakuna aliyeonekana kumfahamu mwanaume ambaye tulikuwa tunamtafuta. Nilipata msukumo wa kusali kumwomba Baba wa Mbinguni msaada.

Baada ya kusali, nilipata hisia kwamba tungempata mwanauume ambaye tulikuwa tunamtafuta, kwa hivyo tuliongeza juhudi zetu. Bado, hatukumpata. Tulichoka na kuamua kurudi katika eneo letu la kuhubiri kwa sababu tulikuwa na miadi mingine. Wakati tulipofika kwenye uwanja wa tekisi, dereva wa tekisi ambaye alikuwa ametuleta katika kijiji aliona nyuso zetu za masikitiko na kutuuliza kama tulimpata yule ambaye tulikuwa tunamtafuta. Jibu letu lilikuwa, bila shaka, la!

Alipendekeza kwamba twende ndani ya shule iliyokuwa pembeni na tuulizie hapo. Tulimwelezea kwamba hayo si maelezo ambayo tulikuwa tumepewa, lakini alisisitiza. Tulishuka kutoka ndani ya tekisi na kuelekea shuleni—sio kwa sababu tulidhani kwamba tungempata mtu yeyote, lakini kumfurahisha tu rafiki yetu aliyekuwa na wasiwasi.

Wakati tulipoanza kutembea kuelekea katika jengo la utawala la shule, mvulana mdogo alikuja akikimbia upande wetu. Alitabasamu na kutuambia kwamba yeye na kaka yake ndio waumini pekee wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho wanaoishi katika eneo hilo na kwamba angeweza kutusaidia.

Mimi na mwenza wangu tuliangaliana kwa mshangao. Ilikuwa ni muujiza. Mvulana huyo alitusaidia kumpata mwanaume ambaye tulikuwa tunamtafuta, na mwishowe alikubali injili na kubatizwa.

Tukio hili lilinifundisha kwamba Baba wa Mbinguni hujibu sala kwa muda Wake na kwa njia Yake mwenyewe. Wakati tunapokosa kupata majibu ya sala zetu mara moja, tunaweza kuwa na imani Kwake na kuwa wavumilivu. ■

*Mwandishi anaishi Jimbo la Rivers, Nigeria.*



Na Mzee Edward Dube

Wa Sabini

# Kupata Imani

Yangu  
Hatua Baada  
ya Hatua

*Kupata ushuhuda inachukua muda. Kawaida inachukua matukio madogo yanayokuja pamoja.*

**M**ojawapo ya nyakati muhimu sana katika maisha yangu ilikuwa wakati nikiwa na umri wa miaka 10 wakati nilipotumia wiki mbili kujifunza mafundisho ya Wakatoliki katika misheni ya Loreto Roman Catholic, takriban maili 20 (32 km) mbali na nyumbani kwetu kijijini Silobela, Zimbabwe. Nimekuja kumjua na kumpenda Mwokozi Yesu Kristo na kumtegemea Bwana kupitia masomo na misukumo hii ya awali.

Wakati nilipokuwa katika kanisa la Katoliki, niliona michoro yenye mandhari kutoka Maisha ya Mwokozi ikining'inia kwenye ukuta: mandhari ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, kufundisha hekaluni, kusali katika Bustani ya Gethsemane, akibeba msalaba kuelekea Kalvari, akisulubiwa Golgotha, na Kufufuka Kwake. Nilihuzunishwa sana kuona misumari na miiba hiyo. Wakati nilipofikia mchoro wa Kusulubiwa, macho yangu yalikuwa yamejawa na machozi. Na kila wakati ningelia na kusema, "Ala, kwa kweli alivumilia mengi, kwa ajili yangu."

Wakati wa sherehe ya uthibitisho, mmoja wa makasisi alinitazama machoni na kusema, "Wewe ni nuru ya ulimwengu" (ona Mathayo 5:14). Kisha, akionesha mshumaa uliokuwa ukiwaka, alidondoa maneno ya Mwokozi: "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele za watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuzze Baba yenu aliye mbinguni." (Mathayo 5:16).

Nilipojifunza zaidi kuhusu Yesu, nilianza kutaka kuwa mwenye huduma kwa wengine. Kwa mfano, tulihitajika kuteka maji yetu zaidi ya maili tano (8 km) kutoka kijijini kwetu. Kwa kawaida, wanawake katika kijiji, ikijumuisha mama yangu, wangebeba mtungi wa lita 20 uliojaa maji juu ya vichwa vyao. Baada ya uzoefu wangu katika seminari ya Katoliki, mara nyingi nilisukuma mtungi wa lita 200 za maji ili kumsaidia mama yangu, na pia niliwasaidia wajane wengine wawili ambao walikuwa jirani zetu. Ninakumbuka hisia nzuri niliyohisi kila wakati nikiwasaidia wengine.

Uzoefu huu ulisaidia kujenga imani yangu katika Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo na kwa namna isiyo ya moja kwa moja kunitayarisha kukubali injili ya Yesu Kristo wakati nilipokuwa na miaka 22.

### **KUPOKEA KITABU CHA MORMONI**

Nilikuwa katika wakati wa mabadiliko nchini mwangu. Wazungu walio wachache wakiongozwa na Ian Smith walitangaza uhuru kutoka kwa Uingereza mwaka 1965. Hilo lilichochea vikwazo kutoka kwa Umoja wa Mataifa na kuanzisha miaka ya vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo viliendelea hadi 1980, ambavyo vilipelekea uhuru wa Zimbabwe. Wakati nilipomaliza masomo yangu, nilihamia jijini kufanya kazi na sikuhudhuria kanisa lolote kwa miaka kadhaa.

Siku moja nilikuwa nikicheza na wana wa bosu wangu. Walikuwa na umri wa miaka tisa na saba. Walisema, "Unajua baba yetu ni rais wa tawi katika Kanisa letu." Walifafanua maana ya rais wa tawi na, bila kufikiria, nilisema, "Baba yenu

hataenda mbinguni." Niligundua nilikuwa nimefanya kosa kubwa, na nikafikiria bila tumaini kuhusu kile ambacho ningeweza kusema kwao kuwafanya wasahau matamshi yangu. Mwishoni mwa siku, wakati walipomwona baba yao, walimkimbiliana na kurudia kile ambacho nilikuwa nimesema. Nilidhani ningepoteza kazi yangu.

Bosi wangu alikuwa amenionesha kabla koti kutoka wakati alipokuwa katika jeshi na ambalo lilionesha alikuwa ameuua. Hiyo ndiyo sababu nilisema kile nilichosema. Kwa upole sana, aliniuliza kwa nini nilisema hivyo. Nilisema, "Bosi, kumbuka, uliniambia kwamba uliua vitani. Katika Biblia inasema, "Usiue."

Aliniuliza kanisa nililokuwa nikihudhuria. Nilimwambia kwamba niliwahi kushirikiki katika Kanisa la Kikatoliki lakini sikuwa nimehudhuria kwa miaka saba. Alishirikiki matukio kutoka Agano la Kale kuhusu vita na uhasama, na kisha akanipa nakala ya Kitabu cha Mormoni. Nilifurahia sana kwamba sikuwa nimepoteza kazi yangu.

Alinipa Kitabu cha Mormoni mwaka 1981, lakini sikukisoma au hata kukifungua kwa muda wa miaka miwili. Jumapili moja nilikuwa nimechoshwa wakati rafiki zangu walipokuwa wametoka nje ya mji, kwa hivyo nilikichukua kitabu na kwenda katika kituo cha reli kilichokuwa karibu na kukisoma. Niliposoma siku hiyo, niliweza kuhisi motisha ya kufanya mema, lakini kile kilichonigusa sana baadaye katika usomaji wangu ilikuwa 3 Nefi 11. Nilisoma kuhusu Wanefi walionusurika ambao walishuhudia vita na ghasia, na kisha Mwokozi Yesu Kristo akawatokea.

Taifa langu lilikuwa limepitia vita vyetu wenyewe kwa miaka 15. Baadhi ya watu niliokuwa nimekuwa nao katika kijiji changu walikuwa wameenda vitani na hawakurudi. Wengine walikuwa wamelemazwa maisha yao yote.

Kwa hivyo, nilipokuwa nikisoma kuhusu Wanefi, nilihisi kana kwamba Mwokozi Yesu Kristo alikuwa ananijia wakati Aliposema, "Inukeni na mje kwangu, ili . . . mguse alama za misumari katika mikono yangu na katika miguu yangu, ili mjue mimi ni Mungu wa Israeli, na Mungu wa ulimwengu wote, na nimeuawa kwa ajili

ya dhambi za ulimwengu, (3 Nefi 11:14).

Nilihisi kana kwamba Alikuwa ananitafuta mimi binafsi, na kunialika niende Kwake. Ilinijia kwamba ningeweza kufanya hivi. Ilibadilisha kila kitu.

## KUPATA USHUHUDA WANGU

Ilichukua miezi kadhaa kupata ujasiri wa kwenda kanisani. Nilijua mahali kanisa lilipokuwa, lakini hapakuwa na wamisionari katika tawi letu dogo. Mnamo Februari 1984, niliingia katika kanisa la Kwekwe. Nilitaka kurudi nje. Sikuwa na hakika kama nilistahili na niliketi upande wa nyuma, tayari kukimbia. Baada ya mazoezi ya ufunguzi, rais wa tawi, Mike Allen, alitoa ushuhuda wake kuhusu Mwokozi Yesu Kristo na Kitabu cha Mormoni. Nilihisi kuhusika. Mtu aliyefuatia pia alitoa ushuhuda wake juu ya Mwokozi na Kitabu cha Mormoni, na hivyo ndivyo wa tatu alivyofanya pia. Nilifurahia sana. Sikuwa na ujasiri wa kwenda kwenye mimbari kwa hivyo, nilisimama pale nilipokuwa na kusema, "Nampenda Yesu. Nasoma Kitabu cha Mormoni." Na nikaketi chini. Huo



*Nimejifunza kwamba kuwa mwanafunzi ni mchakato na tunahitaji kuendelea kusonga mbele.*

ulikuwa mwanzo wa ushuhuda wangu.

Shuhuda hizo zilikuwa njia ya Bwana kunifikia kwa sababu ilinisaidia kuhisi kwamba nilikuwa sehemu ya mahali pale. Nilihisi kwamba hawa walikuwa kaka na dada zangu. Katika siku zilizofuata nilisali kwa niaba yao na kwa ajili ya kukubalika. Nilikutana na waumini huko ambao walikuwa wakarimu mno na ambao walinisaidia.

Mengi yalifanyika siku hiyo wakati nilipoingia kanisani. Nawaza ni nini kingetokea kama waumini hao hawangeshiriki shuhuda zao? Huwezi kujua kama kuna mtu fulani anapitia changamoto. Unaposimama na kusema kile unachohisi, inaweza kuwa hasa kile ambacho mtu fulani anahitaji kusikia.

Toa ushuhuda wako kila mara. Mnapofanya hivyo, mnajiiimarisha nyinyi wenyewe na wengine walio karibu yenu. Tetea kile unachojua. Unapofuata

ushauri kutoka kwenye Kitabu cha Mormoni, utamkaribia Mwokozi.

## **MKARIBIE MWOKOZI**

Muda niliotumia katika Misheni ya Loreto Roman Catholic uliniweka katika njia ya kuwa mwanafunzi wa Mwokozi Yesu Kristo. Tangu wakati huo nimejifunza kwamba kuwa mwanafunzi ni mchakato na tunahitaji kusonga mbele licha ya udhaifu na mapungufu yetu. Wakati tunapokubali mwaliko: “Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu” (Mathayo 5:48), tutaendelea kuelekea uzima wa milele “amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni” (ona Mafundisho na Maagano 98:12).

Tunajua njia daima haitakuwa rahisi, na tutakumbana na changamoto kadhaa na kuvunjika moyo katika mchakato, lakini kumtegemea Bwana ni njia ya pekee ya kupata amani katika maisha yetu.

Upatanisho wa Mwokozi Yesu Kristo ni kila kitu kwangu. Najua kwamba Mwokozi anatufikia. Tunahitaji kutazama juu, kumfuata Yeye, na kwenda kuwainua wengine jinsi Anavyokuja kutuina sisi. ■



# Ni nini unasema wakati rafiki zako hawaamini kwamba Ono la Kwanza lilitokea?

*“Kupitia ufunuo binafsi, unaweza kupokea ushahidi wako mwenyewe kwamba Kitabu cha Mormoni ni neno la Mungu, kwamba Joseph Smith ni nabii, na kwamba hili ni Kanisa la Bwana. Bila kujali nini wengine wanaweza kusema au kufanya, hakuna hata mmoja anayeweza kamwe kuutoa ushahidi ulioshuhudiwa kwenye moyo wako na akili kuhusu nini ni kweli.”*

Rais Russell M. Nelson, “Ufunuo kwa ajili ya Kanisa, Ufunuo kwa ajili Ya Maisha Yetu,” *Liahona*, Mei 2018, 95.



## **Kuza imani**

Pamoja na maswali ya kiroho, si tu mantiki pekee tunayohitaji; pia tunahitaji imani ili kujua kwamba

Ono la Kwanza lingeweza kwa hakika kutokea. Tunaweza kukuza imani hiyo kupitia kumuomba Baba wa Mbinguni na kumsikiliza Roho.

*Julia B., miaka 17, California, Marekani*

## **Jifunze Biblia**

Waombe rafiki zako wajifunze Biblia. Kama wataimini kama neno la Mungu, basi ni sharti waamini kwamba Mungu huzungumza nasi leo kupitia maono kama vile Ono la Kwanza kwa sababu Alifanya hivyo kwa Adamu, Musa, Isaya, na manabii wengine kwa njia tofauti.

*Mzee Muanda, miaka 22, Misheni ya Kenya Nairobi*



## **Muombe Mungu**

Ukweli kwamba ukengefu ulidumu kwa muda wa mamia ya miaka haimanishi kwamba Mungu

alisitisha maono Yake. Tunahitaji kuwa na moyo mnyenyekevu na kumuomba Mungu kwa kusudi halisi na moyo wa kweli, jinsi alivyofanya Joseph Smith.

*Jeremi E., miaka 19, Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo*





### Mwamini Mungu

Ningewauliza rafiki zangu, “Unaamini katika Mungu? Unaamini kwamba aliu-mba vitu vyote? Unaamini kwamba aliwatokea manabii katika siku za kale? Na kama unaamini, kwa nini huamini kwamba inawezekana hivi sasa? Inawezekana!”

*Sarah M., miaka 16, Utah, Marekani*

### Shiriki Ushuhuda Wako.

Ninashiriki ushuhuda wangu pamoja na rafiki zangu kwamba Baba wa Mbinguni hufunua vitu kwa Watoto Wake wakati wanapomwomba Yeye kwa moyo wa kweli ili kujua ukweli. Joseph Smith alikuwa na tamaa ya kujua ukweli, na alitenda kulingana na imani yake. Unaweza pia kufurahia uzoefu wa ajabu kama utamwomba Baba wa Mbinguni kupitia sala kwa moyo wako wote.

*Mara C., miaka 20, Lima, Peru*

*Majibu yanaweza kuhaririwa kwa ajili ya urefu au ufafanuzi. Majibu yaliyochapishwa yanakusudiwa kwa ajili ya msaada na mtazamo, si kama matamko rasmi ya mafundisho ya Kanisa.*

### Unafikiria Nini?

“Ninapata ugumu kuelewana na wazazi wangu. Naweza kuboresha uhusiano wetu?”

Wasilisha jibu lako na, ukipenda, picha ya ubora wa hali ya juu kabla ya Mei 15, 2020, nenda kwenye [liahona.ChurchofJesusChrist.org](https://www.liahona.churchofjesuschrist.org) (bofya “Wasilisha Makala au Maoni”). Au tuma barua pepe ya majibu yako kwa [liahona.ChurchofJesusChrist.org](https://www.liahona.churchofjesuschrist.org).



## Ni kwa jinsi gani Joseph Smith alitafsiri Kitabu cha Mormoni?

Kabla ya kuficha bamba za dhahabu, Moroni, nabii wa mwisho katika Kitabu cha Mormoni, aliandika kwenye ukurasa wa jina wa kitabu kwamba kitabu kingetafsiriwa “kupitia karama na uwezo wa Mungu.” Haya yanabakia kuwa maelezo bora zaidi ya tafsiri ya Kitabu cha Mormoni.

Joseph Smith alisoma kwa sauti maneno ya tafsiri kwa maandishi, hasa Oliver Cowdery. Kwa sababu Joseph alikuwa akitafsiri lugha isiyojulikana kabisa, alihitaji msaada wa Bwana. Njia moja ambayo Bwana alitoa msaada ilikuwa kutoa vifaa kumsaidia Joseph katika kutafsiri. Mashahidi walisema kwamba Joseph aliangalia kwa kutumia vifaa na kwamba maneno yalio- nekana kwake kwa Kingereza. Vifaa vya kutafsiri vilijumuisha “vikalimani” au “Urimu na Thumimu”—mawe mawili masafi ambayo yalikuwa yame- wekwa katika pinde ili Joseph aweze kutazama ndani yake. Hivi vilikuwa vimekabidhiwa kwa Joseph Smith pamoja na mabamba. Kifaa kingine ambacho Joseph alitumia kilikuwa “jiwe la mwonaji” ambalo angeanga- lia kupitia hilo, kawaida kwa kuliweka ndani ya kofia. Joseph alikuwa amelipata jiwe hili awali na akawa amelitumia kupata vitu vilivyofichika au vilivyopotea. Alitumia vyote viwili vikalimani na jiwe la mwonaji wakati akitafsiri, siku zote akitegemea msukumo kutoka mbinguni.

Kutafsiri Kitabu cha Mormoni ilikuwa kwa kweli muujiza na kulifanyika “kwa karama na uwezo wa Mungu.”

**Kwa maelezo zaidi kuhusu kutafsiriwa kwa Kitabu cha Mormoni, ona “Kutafsiri Kitabu cha Mormoni” kwenye [topics.ChurchofJesusChrist.org](https://topics.churchofjesuschrist.org) au katika Mada za Injili katika Gospel Library app.**

# Picha Nne kutoka

# WIKI YA PASAKA

## Taji ya Miiba

**Ona Mathayo 27:29; Marko 15:17; Yohana 19:2.**

Wanajeshi Warumi walimvisha Mwokozi taji ya miiba. "Pengine kitendo hiki cha ukatili kilikuwa jaribio la ukaidi la kuiga kumvika heshima mfalme mkuu juu ya kichwa Chake. . . Ni uchungu ulioje, ukizingatia kwamba miiba iliashiria kero ya Mungu wakati alipoilaani ardhi kwa ajili ya Adamu kwamba kuanzia wakati huo ingezea miiba. Lakini kwa kuivaa taji hiyo, Yesu aliibadili miiba kuwa ishara ya utukufu Wake" (Rais James E. Faust, Apr. 1991 mkutano mkuu).



**"Ufalme Wangu sio wa ulimwengu huu"**  
(Yohana 18:36).



## Joho la Rangi ya Zambarau

**Ona Mathayo 27:28; Marko 15:17; Yohana 19:2.**

Zambarau ilikuwa rangi ya kifalme, na wanajeshi walimvisha Yesu Kristo joho hili kwa dhuhaka kwa sababu alikuwa amekiri kuwa mfalme wa Wayahudi. Bila shaka, kwa kweli Yeye ni zaidi ya hilo—Yeye ni "Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana" (1 Timotheo 6:15; Ufunuo 19:16).

**"Damu inatiririka kutoka kwenye kila kinyweleo, mateso yake yatakuwa makuu"**  
(Mosia 3:7).

## Kisindiko cha Mzeituni

**Ona Mathayo 26:36; Marko 14:32; Luka 22:39-40; Yohana 18:1.**

“Ni ishara ya kina kwamba ‘damu [ilitiririka] kutoka kila kinyweleo’ [Mosia 3:7] wakati Yesu akiteseka katika Gethsemene, mahali pa kisindiko cha mzeituni. Ili kuzalisha mafuta ya mzeituni nyakati za Mwokozi, mizeituni kwanza ilipondwa kwa kuwekewa jiwe kubwa juu yake. “Rojorojo” iliyofanyika kisha iliwekwa kwenye vikapu laini vya kusukwa vyenye matundu, ambavyo viliwekwa kimoja juu ya kingine. Uzito wa mrundikano huu ulikamua mafuta ya kwanza na safi. Halafu mkamuo ukaongezwa kwa kuwekewa nguzo kubwa au gogo juu ya mrundikano ule wa vikapu, na kutoa mafuta mengi zaidi. Mwishoni kabisa, ili kutoa mafuta ya mwisho, nguzo au gogo liliwekewa mawe juu yake kwenye upande mmoja ili kuleta mkandamizo na kukamua zaidi. Na ndiyo, mafuta ni mekundu kama damu wakati yanatoka” (Mzee D. Todd Christofferson, Okt. 2016 mkutano mkuu).



## Kaburi Wazi.

**Ona Mathayo 28:1-8; Yohana 20:1-18.**

“Kaburi wazi asubuhi ile ya kwanza ya Pasaka lilikuwa jibu la swali la Ayubu, “Mtu akifa, je! Atakuwa hai tena?” [Ayubu 14:14]. Kwa wote wanaoisikia sauti yangu, ninatangaza, Mtu akifa, atakuwa hai tena. Tunajua, kwani tuna nuru ya ukweli uliofunuliwa” (Rais Thomas S. Monson, “Amefufuka!” Apr. 2010 mkutano mkuu).

“Hayupo hapa,  
amefufuka”  
(Luka 24:6).



## LENGO LAKO NI NINI?

*Kama vijana wakubwa,  
kila mmoja wetu ana jukumu  
katika Urejesho unaoendelea.  
Unashiriki kwa jinsi gani?*

42



VIJANA

**USHUHUDA WAKO  
WA ONO LA KWANZA**

52, 62

PASAKA

**PICHA NNE**

64

KWA WATOTO

**SOMA HADITHI YA  
UREJESHO**

R4

KANISA LA  
**YESU KRISTO**  
LA WATAKATIFU  
WA SIKU ZA MWISHO



SWAHILI

# Rafiki



Yesu Kristo Yu Hai  
na Alirejesha  
**KANISA** Lake!





Na Rais  
Russell M.  
Nelson

# Kutoa msaada kwa UREJESHO

Mwaka 1820, Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo walimtokea Joseph Smith. Baba wa Mbinguni alisema, “Huyu ni Mwanangu Mpendwa. Msikilize Yeye!” Urejesho wa injili ulianza siku hiyo miaka 200 iliyopita. Unaendelea leo!

Siku moja Yesu Kristo atarudi duniani tena. Hizi ni njia nne unazoweza kutoa msaada kwa Urejesho na kujitayarisha kwa ajili ya wakati ambapo Yesu atarudi:

- Jenga imani yako katika Yesu Kristo.
- Fanya uchunguzi kuhusu familia yako na toa msaada ili kazi ya hekaluni ifanywe kwa niaba yao.
- Jiandae kwenda hekaluni.
- Wasaidie watu wajifunze kuhusu Yesu Kristo na Kanisa Lake.

Kufanya vitu hivi kutasaidia kuandaa ulimwengu kwa ajili ya siku ya kupendeza wakati Yesu atakaporudi tena. ●



*Imetoholewa kutoka “Hope of Israel” (ibada ya vijana kote ulimwenguni, Juni 3, 2018), 19, HopeOfIsrael.ChurchofJesusChrist.org.*

Rais Nelson alisema watoto wanaweza kutoa msaada kwa Urejesho. Ni njia gani moja ambayo unaweza kutoa msaada?

## Kujifunza kuhusu Urejesho


Wamisionari wanaifundisha familia hii kuhusu jinsi injili ya Yesu Kristo ilivyorejeshwa. Tafuta vipengele vilivyo hapa chini ambavyo vinawakilisha sehemu za Urejesho.



VIELEZO NA CARLES MARTI



Neno la Hekima



sakramenti



kazi ya umisionari



maandiko



kipawa cha Roho Mtakatifu



mahekalu



historia ya familia



kanisa



ukuhani

Fungua ukurasa mpya ujifunze zaidi kuhusu Urejesho!

# Kanisa la Yesu Kristo Limerejeshwa!



Kabla ya kuja duniani, tuliishi pamoja na Wazazi wa Mbinguni. Walitupenda! Baba wa Mbinguni alikuwa na mpango wa kupendeza kwa ajili yetu. Tungekuja duniani ili tuweze kupata mwili na kujifunza na kukua. Kisha tungeweza kurudi kuishi nyumbani kwetu mbinguni. Lakini hatungeweza kufanya hivyo peke yetu. Tungehitaji usaidizi.



Baba wa Mbinguni alimchagua kaka yetu mkubwa, Yesu Kristo, aje duniani kutusaidia. Yesu alituaonesha jinsi ya kuwapenda wengine na kufuata amri za Baba wa Mbinguni. Aliwachagua Mitume waliongoze Kanisa Lake.



Yesu Aliteseka kwa ajili yetu katika Bustani ya Gethsemane. Alihisi uchungu na huzuni yetu yote. Alikufa msalabani kwa ajili yetu. Kwa sababu ya hili, tunaweza kwenda Kwake wakati tumeumia au tuna huzuni au tunahitaji msaada. Tunaweza kutubu wakati tunapofanya makosa.



Siku ya tatu baada ya Yesu kufa, alifufuka. Yesu alikuwa hai tena! Kwa sababu hili, sisi pia tutafufuliwa. Tunaweza kuishi mbinguni tena baada ya sisi kufa.



Baada kufufuka Kwake, Yesu aliwatembelea wafuasi Wake huko Amerika. Aliwaomba Mitume Wake waendeleo kufundisha watu kuhusu injili Yake. Watu wengi waliowasikiliza Mitume walibatizwa na kujiunga na Kanisa.



Baada ya Mitume kufariki, watu walianza kusahau baadhi ya vipengee muhimu vya injili ya Yesu. Waliacha kuamini kwamba Baba wa Mbinguni siku zote angewavuvia watoto wake duniani. Walisahau kwamba kila mtu duniani angekuwa na nafasi ya kubatizwa. Waliacha kuamini kwamba manabii na mitume daima wangeongoza Kanisa.



Miaka mingi ilipita. Hatimaye, ilifika wakati wa kurudisha vipengee vilivyopotea katika injili ya Yesu. Ilikuwa wakati wa kurejesha Kanisa Lake! Baba wa Mbinguni alihitaji mtu awe nabii na asaidie kulirejesha duniani. Alimchagua mvulana mdogo aliyeitwa Joseph Smith.





Siku moja, Joseph alikuwa akisoma Biblia. Katika Yakobo 1:5, ilisema kwamba Baba wa Mbinguni atajibu maswali yetu wakati tunapouliza kwa imani. Joseph alikuwa na swali! Alijua kulikuwa na makanisa mengi ambayo yalifundisha kuhusu Yesu. Lakini alitaka kujua kama kulikuwa na moja kama vile Kanisa la Yesu katika Agano Jipya.

Katika siku nzuri ya majira ya kuchipua karibia na Pasaka, Joseph alikwenda msituni karibu na nyumbani kwao. Alipiga magoti na kuanza kusali. Kisha Joseph akahisi hisia ya giza. Shetani alikuwa anajaribu kumvunja moyo. Lakini Joseph aliendelea kusali kwa uwezo wake wote.




Kisha nuru nzuri ikashuka chini. Joseph aliwaona Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo. Hii inaitwa Ono la Kwanza. Walisema kwamba Kanisa la Yesu Kristo halikuwepo duniani. Lakini lingekuwapo karibuni. Urejesho ulikuwa unaanza!



Baba wa Mbinguni aliwatuma malaika kurejesha vipengele muhimu vya injili. Malaika Moroni alimpatia Joseph bamba za dhababu ili tuweze kupata Kitabu cha Mormoni kutusaidia kujifunza kuhusu Yesu Kristo.



Yohana Mbatizaji alirejesha Ukuhani wa Haruni ili tuweze kubatizwa. Petro, Yakobo, na Yohana wali-leta ukuhani wa Melkizedeki ili tuweze kupokea Roho Mtakatifu na kupata baraka wakati tunapougua.




Eliya alikuja ili tuweze kuunganishwa na familia zetu hekaluni.




Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho lilianzishwa. Hii inamaanisha kwamba Kanisa la Yesu limerejea duniani! Vitu hivi vyote ni sehemu za Urejesho.

Urejesho wa Injili ungali unaendelea leo hii. Manabii, mitume, wamisionari, na waumini wanashiriki habari njema ya Yesu Kristo kote ulimwenguni. Mahekalu yanajengwa katika nchi nyingi ili watu waweze kuunganishwa na familia zao milele. Na kanisa linawasaidia watu katika maeneo ambayo kuna njaa au maafa.



Kila mtu anaweza kufanya kitu kutoa msaada kwa Urejesho. Unaweza kusaidia kwa kujifunza kuhusu historia ya familia yako na kufanya ubatizo wa hekaluni. Unaweza kutoa zaka kujenga makanisa na mahekalu. Unaweza kutoa matoleo ya mfungo kuwasaidia watu wenye mahitaji. Unaweza kuwaelezea watu kuhusu Yesu Kristo.



Yesu Kristo alitupatia Kanisa Lake kutusaidia sisi kurudi kwa nyumbani kwetu mbinguni. Tunaweza kushiriki sakramenti na daima kukumbuka kile Alichofanya kwa niaba Yetu. Tunawezaje kuonesha upendo kwa wengine, kama Alivyofanya. Tunaweza kumsaidia kila mtu kujifunza kuhusu injili yake! ●

# Itafute!

Kwa sababu ya Urejesho, leo watu kote ulimwenguni wanaweza kufahamu kuhusu injili ya Yesu Kristo!  
Ni nakala ngapi za Kitabu cha Mormoni unaweza kuzipata? Ni bendera ngapi za nchi mbali mbali unaweza kuzipata?  
Changamoto ya ziada: Je, unatambua bendera yoyote?



# Baba wa M Husikia Sa

Baba wa Mbinguni alisikia  
Yeye husikia y





# Mbinguni la Zangu

na sala ya Joseph Smith.  
yangu pia!





# Kanisa kwa ajili ya Zulma

*Pengine kulikuwa na zaidi ambayo  
Mungu alitaka Zulma aelewe.*

**Na Lucy Stevenson**

Magazeti ya Kanisa  
(Imetokana na hadithi ya kweli)

*“Tafuteni, na mtapata”*

*(3 Nefi 14:7).*

Zulma aliketi kwenye mojawapo ya benchi za Kanisa na kunyosha sketi ya sare zake za shule.

Mwangaza wenye rangi tofauti

uling'aa kupitia madirisha yenye

vioo vya rangi, na msalaba ulisimama mbele ya kanisa.

Zulma alisomea katika shule ya kanisa, kwa hivyo alihudhuria ibada mara mbili kwa siku

pamoja na wanafunzi wengine. Zulma alipenda Kanisa.

Alimpenda Yesu na alipenda kujifunza juu Yake.

Aliketi kwa utulivu wakati kasisi alipoanza kuzungumza. Lakini leo alihisi kitu tofauti. Ghafla wazo jipya lilimjia akilini na moyoni mwake: *Kuna ukweli zaidi huko nje.*

Zulma alijikuna nyusi. Ukweli Zaidi? Hilo lilimaanisha nini?

Wazo likaja tena. *Kuna ukweli zaidi.*

Zulma alifumba macho na kufokasi kwenye kile alichokuwa akihihi. Alikuwa amejifunza vitu vingi vizuri kanisani. Lakini sasa alijiuliza kama kuna kitu kilichokuwa kinakosa. Pengine kulikuwa na zaidi ambayo Mungu alimtaka afahamu. Lakini angewezaje kuyapata?

Baadaye alizungumza na kaka yake mkubwa, Alberto, kuhusu mawazo yake.

“Unafikiri kuna ukweli zaidi huko nje?” Alberto aliuliza.

Zulma aliitikia kwa kichwa. “Ninataka kujifunza kuhusu makanisa mengine,” alisema.

“Sawa,” Alberto alijibu. “Niteanda pamoja nawe!”

Kwa miaka kadhaa, Zulma na Alberto walitembelea makanisa tofauti. Baada ya ibada katika kanisa moja, Alberto alisema, “Lile Kanisa lilifundisha mambo mazuri.”

Zulma alikubaliana naye, lakini bado walihisi kuna kitu kilikosekana, kwa hivyo waliendelea kutafuta.

Siku moja Alberto alikimbia juu ya ngazi kuelekea nyumbani kwao. “Nimelipata kanisa tulilokuwa tunalitafuta!” Alberto alisema. Alimkumbatia Zulma.



Huyu ni Zulma akiwa msichana mdogo. Mkono wa kulia ni picha yake leo pamoja na mumewe, Mzee Walter F. González wa Sabini.

Macho ya Zulma yalifunguka wazi kabisa. “Wapi? Kivipi?”

“Rafiki yangu alikutana na wamisionari kutoka Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho,” Alberto alisema. “Niliwasikiliza, na ninaamini kile walichofundisha!”

Zulma na Alberto walikuwa na furaha kubwa kwa mba walidensi kuzunguka nyumba. Lakini Zulma akapata habari mbaya. Mamá hakutaka akutane na wamisionari. “Una miaka 12 tu,” Mamá alisema. “Wewe ungali mdogo sana.”

Kwa sababu Alberto alikuwa mkubwa, alikubaliwa kuendelea kukutana na wamisionari. Wiki chache baadaye, alibatizwa.

Zulma aliendelea kumuuliza Mamá tena na tena kama angeweza kujifunza kutoka kwa wamisionari. Hatimaye, Mamá alisema sawa.

Wakati wamisionari walipomfundisha Zulma, alihisi joto moyoni mwake. Mmoja wa wamisionari alikuwa na wakati mgumu kuzungumza Kihispania, lakini hilo halikuwa hoja. Cha muhimu ilikuwa ni jinsi alivyohisi Zulma. Wakati alipojifunza kuhusu Joseph Smith na Kitabu cha Mormoni, alijua alikuwa amepata ukweli aliokuwa akiutafuta!

Zulma alitaka kubatizwa. Lakini Mamá angesema nini? Zulma alifurahia sana wakati Mamá aliposema sawa! Siku ya kubatizwa kwake, Zulma alivalia mavazi meupe. Alijua Mungu Alimpenda. Alijua Alimfahamu. Na alijua kwamba alikuwa amemsaidia kupata Kanisa Lake lililorejeshwa! ●



# Ono la Kwanza

Kwa unyenyekevu ♩ = 68

Maneno na muziki: Nathan Howe

D G D G

D A G A

1. Jo - seph a - li - ho - ji ji - nsi ya ku - fa - nya, Kwa  
 2. Pe - nye u - tu - li - vu, kwe - nye ki - ji - si - tu, A -  
 3. Kwa ma - o - no ya - le, ya - ka - ja me - ngi - ne. Bwa -

F C B $\flat$  A

hi - vyo, kwa bi - di - i a - ka - pe - le - le - za. Ne -  
 ka - mu - o - mba Mu - ngu kwa u - nye - nye - ke - vu. Ba -  
 na a - ka - re - je - sha i - nji - li tu - ju - e: Ha -

D Em E A

no ta - ka - ti - fu li - ka - se - ma sa - li, Na  
 ba na Mwa - na - e wa - ka - shu - ka chi - ni Ku -  
 ja - fu - nga mbi - ngu; Bwa - na a - o - nge - a. Hu -

© 2020 by Nathan Howe. All rights reserved.

Wimbo huu ni kwa matumizi ya kawaida, ya kanisa yasiyo ya kibiashara au matumizi ya nyumbani.

Notisi hii lazima ionekane kwenye kila nakala iliyotolewa.



G Em F#m Bm Em7 A7 D

Jo - seph a - li - ju - a Mu - ngu hu - ji - bu ma - o - mbi.  
 m - ji - bu Jo - seph, pi - a ku - re - je - sha i - nji - li. A - li - o -  
 i - ta na - bi - i ku - tu - fu - ndi - sha Ya - ke nji - a.

D Em F#m Em Bm

mba \_\_\_\_\_ na ku - ji - bi - wa. \_\_\_\_\_ Ba - ba a - li - mwi - ta kwa ji -

A D G A D G

na. \_\_\_\_\_ Na - ju - a a - ni - pe - nda Mu - ngu \_\_\_\_\_ Na

Em A D G D

hu - ni - si - ki - a.



# Hujambo kutoka Msitu Mtakatifu!



**Habari,  
sisi ni Margo  
na Paolo.**



Wakati Joseph Smith alipokuwa na umri wa miaka 14, aliishi katika nyumba ya magogo New York, Marekani. Alikuwa na kaka watano na dada watatu. Aliwatii wazazi wake na alikuwa mwema kwa wengine. Alisoma Biblia pamoja na familia yake, lakini wote hawakushiriki kanisa moja.

**2**

Joseph alikuwa mchapa kazi. Alisaidia kukata miti ili familia yake iweze kupanda mazao. Pia aliisaidia familia yake kukusanya utomvu kutoka kwenye miti ya maple ili kutengeneza sukari.



**Mwezi huu, ili  
kusherehekea Urejesho,  
tunatembelea eneo  
ambapo Ono la Kwanza  
lilitokea miaka  
200 iliyopita!**



**3**

Joseph alitaka kupata Kanisa kama lile la kwenye Biblia. Siku moja alienda katika msitu na kusali. Baba wa Mbinguni na Yesu walimtokea. Walimwambia dhambi zake zilikuwa zimesamehewa. Pia walimwambia kwamba asijiunge na kanisa lolote. Punde Kanisa la Yesu Kristo lingerejeshwa!

**4**

Watu wengi walimfanyia mzaha Joseph kwa ajili ya kile alichooona. Walisema alikuwa akidanganya. Lakini Joseph aliendelea kusema ukweli. Alisema “Nami najua hivyo, nami nilijua kwamba Mungu alijua, na sikuweza kukataa” (Historia ya—Joseph Smith 1:25).

**5**

Leo watu wanaweza kutembelea eneo ambapo Joseph alisali. Ni zuri na la amani.



**Watoto hawa wanaishi mahali  
alipolelewa Joseph Smith!**



Ninajua Msitu Mtakatifu ni mahali maalum kwa sababu Joseph Smith alisali na kuwaa-na Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo pale.

**Piper D., miaka 5,  
New York, Marekani.**



Nina shukrani kwamba tunaishi karibu na nyumbani kwa Joseph Smith. Ninapenda kwenda katika Jengo la Grandin ambalo lina mtambo wa kupiga chapa. Ninapenda sana kuona mahali ambapo walijalidi nakala za mwanzo za Kitabu cha Mormoni.

**Roscoe B., miaka 9,  
New York, Marekani**

**Asante kwa  
kutalii Msitu Mta-  
katifu pamoja nasi.  
Tutaonana wakati  
mwingine!**



# Familia ya Milele ya Alonso

**Na Marissa Widdison**

Magazeti ya Kanisa

(Imetokana na hadithi ya kweli)

*“For the temple is a holy place where we are sealed together” (Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 95).*

**P**asaka ni wakati mzuri wa kufikiria kuhusu Yesu na kukumbuka Ufufuo Wake,” Dada Rojas alisema. Alishikilia juu picha ya Yesu. “Kwa sababu Yake, watu waliofariki wataishi tena.”

Alonso aliinua kichwa chake wakati mwalimu wake wa Msingi aliposema hivyo. *Je, hiyo inamaanisha kwamba naweza kuwaona wazazi wangu tena?* Alonso aliwaza.

Mamá alifariki miaka mingi iliyopita. Alonso hakumkumbuka vizuri, lakini alipenda kuona picha zake. Kisha Papá akafariki pia.

Sasa Alonso aliishi na Abuela, bibi yake. Alikuwa anamfundisha kuhusu Kanisa lake, Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Angebatizwa na kuthibitishwa mwaka ujao, wakati ambapo angefikisha umri unaofaa.

Kisha Dada Rogers akashikilia juu picha ya jengo jeupe. “Zawadi nyingine ya kupendeza kutoka kwa Yesu Kristo ni mahekalu. Hili ni mojawapo ya mahekalu hapa Chile.”

Alonso alitazama sanamu ya dhahabu juu ya jengo. Ilikuwa ya kupendeza! Aliwaza ni nini kinafanyika ndani yake.

“Naweza kuwa na Mamá na Papá tena?”





“Mahekalu ni mahali familia zinapounganishwa milele,” Dada Rojas alisema. “Hekalu hili kule Santiago ni mahali nilipounganishwa na wazazi wangu baada ya kujiunga na Kanisa. Kwa sababu tuliunganishwa, naweza kuwa nao hata baada ya maisha haya.”

Alonso alisisimka wakati aliposikia hilo.

“Naweza kuunganishwa na wazazi wangu?” aliuliza.

“Hata kama tayari wameaga dunia?”

Dada Rojas aliitikia kwa kichwa. “Ndiyo! Hiyo ndiyo mojawapo ya sababu ya mahekalu kuwa muhimu sana. Yanawabariki wanafamilia wetu wote, ikiwa ni pamoja na wale ambao wameaga dunia.”

Kwa muda uliosalia kwa siku hiyo, Alonso aliendelea kufikiria juu ya mahekalu. Alimuomba Abuela amfundishe zaidi. Alizungumza kuhusu mavazi meupe ambayo watu huvalia ndani na kazi ya sanaa ya kupendeza kwenye kuta.

“Kizuri zaidi ya yote, ni mahali ambapo unaweza kuunganishwa na wazazi wako,” Abuela alisema.

“Tutawaomba watu wawili kutoka katika kata kuwawakilisha wakati wa kuunganisha.”

“Tunaweza kwenda kesho?” Alonso aliuliza. “Nataka kuwa na Mamá na Papá milele!”

Abuela alitabasamu. “Nina furaha unataka kwenda,” alisema. “Lakini hekalu lililo karibu nasi ni Concepción. Hatuna hela za kutosha kwa ajili ya tiketi za basi.”

“Nitasaidia kuweka akiba kwa ajili ya safari!”

Alonso alisema.

Kuanzia hapo, wakati wowote Alonso alipopata senti mtaani au kupata nafasi ya kupata pesa, alilipa zaka na kisha kuongeza zilizobaki kwenye hazina yao ya hekaluni.

Baada ya miezi mingi ya kuweka akiba, Alonso na Abuela hatimaye walikuwa na hela za kutosha kusafiri kwenda hekaluni. Waliwaomba Kaka na Dada Silva kwenda nao. Siku ya safari, walisafiri kwa muda mrefu wakitumia basi kwenda katika jiji la Concepción. Ilikuwa inakaribia machweo wakati Alonso alipoona kitu chenye rangi ya dhahabu kwa mbali.



“Naweza kumuona malaika Moroni!” Alonso alisema, aki-onesha sanamu iliyokuwa juu ya paa la kuba lenye rangi ya samawati.

Walilala katika ghorofa iliyokuwa kando ya hekalu. Asubuhi, Alonso aliingia ndani ya hekalu kwa mara ya kwanza. Aliona picha kubwa ya Yesu ndani. Yeye na abuela walivalia mavazi meupe. Alihisi furaha na amani.

Ilipowadia wakati wa kuunganishwa, Alonso aliingia ndani ya chumba kizuri kilichopambwa kwa vioo kwenye kuta. Mhudumu wa hekaluni alimwonesha Alonso, Abuela, na kina Silva jinsi ya kupiga magoti wakizunguka meza maalum inayoitwa madhabahu. Ilikuwa imefunikwa kwa kitambaa laini.

Kaka na Dada Silva walikuwepo kwa niaba ya mama na baba wa Alonso. Abuela alikuwepo kwa niaba ya dada yake aliyeaga dunia kabla ya Alonso kuzaliwa.

Akiwa amefumba macho yake, Alonso alipata taswira ya familia yake ikiwa pamoja.

*Siwezi kungoja kuwaona tena, Alonso aliwaza. Nina shukrani sana kwamba familia zinaweza kuwa pamoja milele! ●*





**Na Dada Joy D. Jones**  
Rais Mkuu wa Msingi

# Hekalu na WEWE



**K**abla ya kurejeshwa kwa Kanisa, watu waliamini kwamba ikiwa mtu fulani katika familia yao alifariiki bila ya kubatizwa, hawangemuona tena. Lakini kwa sababu ya Urejesho, tunaweza kubatizwa kwa niaba yao katika hekalu. Tunaweza kuunganishwa pamoja milele!

Kama Joseph Smith, wewe pia umechaguliwa na Baba wa Mbinguni kufanya kazi muhimu maishani mwako. Baadhi ya kazi hiyo inaweza kufanyika katika mahekalu. Unaweza kukusanya majina ya mababu zako ambao hawakubatizwa wakati walipoishi duniani. Kisha, baada ya kupokea kibali cha hekaluni, unaweza kwenda hekaluni na kubatizwa kwa niaba yao.

Unapofanya kazi hii, sali kwa Baba wa Mbinguni

akuongoze. Mababu zako wanaweza kukusaidia pia. Ni baraka muhimu na takatifu iliyoje hii itakuwa kwa ajili yako na kwa ajili yao!

Baadhi yenu mnaweza kuwa hamuwezi kufanya kazi ya hekaluni kwa wakati huu, lakini siku moja mtaweza. Kumbuka siku zote kwamba wewe ni mtoto wa Mungu. Yeye anakupenda kikamilifu.

Sikiliza uvuvio wa Roho Mtakatifu na kuwa tayari kwenda hekaluni siku moja. Kufanya hili kutakusaidia kujenga maisha mazuri kwa ajili yako na kwa ajili ya familia zako za awali, za wakati huu, na za baadaye. Unapofanya kazi ya Bwana, Yeye atakusaidia. Wewe ni mmoja wa roho Zake jasiri zaidi. ●



Wewe ni mtoto mpendwa wa Mungu, unayejulikana Kwake na unayependwa Naye. Mungu alimjua Joseph Smith. Hilo pia ni kweli kwako. Mungu anakujua.

Mzee Dale G. Renlund wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili  
Imetoholewa kutoka "Baraka ya Urejesho kwa ajili Yako," *Liahona*, Feb. 2020, 52.

# Wapendwa Wazazi,

Mapema msimu wa kichipua mwaka 1820, karibu na wakati wa Pasaka, Joseph Smith aliomba na kuwaona Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo. Gazeti hili linazungumza kuhusu wakati huo maalum. Hizi ni kurasa chache za kutafuta:

- Hadithi inayosimuliwa kwa picha inaelezea jinsi ambavyo Kanisa Lililorejeshwa ni sehemu ya mpango wa Mungu (R4–10).
- Rais Nelson anatumia jinsi ambavyo tunaweza kutoa msaada kwa Urejesho (R2).
- Wimbo mpya unafundisha kuhusu Ono la Kwanza (R16–17).
- Hadithi inafundisha jinsi Urejesho unavyoweza kubariki familia zetu (R20–21).

Je, si inapendeza kwamba tunaweza kuwa wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho? Acheni tushiriki habari njema ya Yesu na Kanisa Lake kwa ulimwengu!

Pasaka Njema,

*Rafiki*

## JINZI YA KUTUMA KAZI YA SANAA YA MTOTO WAKO AU UZOEFU KWENYE LIAHONA

Nenda kwenye [liahona.ChurchofJesusChrist.org](http://liahona.ChurchofJesusChrist.org) na bofya "Wasilisha Makala au Majibu." Au itume kwetu kupitia barua pepe [liahona@ChurchofJesusChrist.org](mailto:liahona@ChurchofJesusChrist.org) likiwemo jina la mtoto wako, umri, jiji la makazi, na maelezo haya ya ruhusa: "Mimi, [ingiza jina lako], natoa ruhusa kwa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho kutumia wasilisho la mtoto wangu kwenye magazeti ya Kanisa, kwenye mitandao ya Kanisa na kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii, na yamkini katika nyenzo zingine za Kanisa." Tuna hamu ya kusikia kutoka kwako!



**Tafuta Liahona iliyofichwa ndani!**

## YALIYOMO

- R2** Kutoka kwa Urais wa Kwanza: Kutoa Msaada kwa Urejesho
- R4** Kanisa la Yesu Kristo Limerejeshwa!
- R11** Vitu vya Kuburudisha: Itafute!
- R12** Ukurasa wa Kupaka Rangi
- R14** Kanisa kwa ajili ya Zulma
- R16** Muziki: Ono La Kwanza
- R18** Hujambo kutoka katika Msitu Mtakatifu!
- R20** Familia ya Milele ya Alonso
- R22** Hekalu na Wewe
- R23** Wazo Zuri